# Nipashe

Alhamisi Aprili 15, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580551

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710


ama
AFYA NA MAZINGIRA
Tumeboresha hivi nyendo za maji kwa mchoro wa 1980
MTETEZI CONSOLATHA:
Fahamu orodha ya ukatili wapatao kinamama walioko kazini sokoni

UKURASA 11

**MAKAMBA** ataka wakosoa serikali wasiitwe wasaliti

UK. 2



**HOSEAH** ajinadi kwa nini anafaa kuwa Rais TLS

UK. 8

# Ajira 2,000 kumwagwa Afya

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**WALIOFARIKI DUNIA SAME WAFIKIA 11**

IDADI ya watu waliofariki dunia katika ajali ya gari iliyohusisha basi dogo la abiria aina ya Toyota Hiace na Toyota Alphard...

UKURASA WA 3

**MWANAFUNZI DARASA LA NNE AJINYONGA HADI KUFA**

MWANAFUNZI wa darasa la nne Shule ya Msingi Muungano, wilayani Tunduru, mkoani Ruvuma, Abdul Abubakar (12)...

**Mlipuko baruti waua na kujeruhi**

UKURASA 2

## **Walimu** nao mkao wa kula ajira 6,000, ni mkakati wa kuajiri watumishi 40,000...

*Endelea Uk. 2*



Rais Samia Suluhu Hassan, akifanya mazungumzo na Makamu wa Rais, Dk. Philip Isdor Mpango, Ikulu jijini Dodoma jana. PICHA: OMR . **PICHA: IKULU**



## MAHOJIANO MAALUM:

# Msekwa afunguka kuhusu Rais Samia

UK. 4



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

MICHEZO TIKETI KOMBE DUNIA YAMPAGAWISHA PAWASA UK.23

MAONI, KATUNI UK.6



Mbunge wa Bumbuli, Januari Makamba, akichangia bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu ya mwaka 2021/2022, bungeni jijini Dodoma, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ajira 2,000 zaidi kumwagwa Afya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema iko mbioni kutangaza ajira 2,161 za kada ya afya hivi karibuni ili kupunguza uhaba wa watumishi wa afya.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa, alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akifungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa wizara hiyo, jijini hapa.

Alisema kibali cha ajira hizo kinaendelea kushughulikiwa sambamba na ajira za walimu 6,000.

"Ajira hizi tutazitangaza hivi karibuni, mpango wetu wa serikali ni kuhakikisha kwa mwaka 2020/21 tunaajiri watumishi 40,737, kwa namna ambavyo bajeti itaruhusu," alisema.

Alisisitiza serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan itaendelea kutoa kipaumbele cha ajira kwa watumishi wa umma na vibali vya ajira ili kuziba nafasi zilizoachwa wazi kutokana na watumishi kustaafu, kufariki au kuacha kazi kwasababu mbalimbali.

"Katika ajira hizo kwa mwaka 2020/21 kipaumbele kimetolewa kwenye kada zenye upungufu mkubwa wa watumishi ni pamoja na walimu wa sayansi, hisabati, ufundi sanifu na maabara," alisema.

Alisema kwa upande wa afya kipaumbele ni kuajiri madaktari, wauguzi, wataalamu wa lishe, wataalam wa ugani, nishati, mafuta na gesi.

"Serikali itaendelea kutenga bajeti kila mwaka kutoa ajira mpya na ajira mbadala ili kuimarisha utendaji wa serikali katika sekta mbalimbali," alisema.

Kuhusu upandishaji vyeo na nyongeza ya mishahara kwa watumishi wa umma, Waziri Mchengerwa alisema hivi karibuni kuna watumishi walipanda madaraja, lakini upatikanaji wa takwimu zao umekuwa mgumu.

"Watumishi wanashindwa kupata nyongeza zao za mshahara kutokana na maofisa utumishi wameshindwa kutuletea idadi yao na sisi serikali tumesema katika bajeti ijayo lazima tuwasaidie wapandishe madaraja na tofauti ya madaraja ionekane kwenye salary slip zao na hii ndio tofauti ya serikali ya awamu ya sita, tumejikita moja kwa moja kutatua kero za watumishi," alisema.

Alisema ofisi yake inaendelea kuandaa takwimu hizo na kuomba kibali kwa rais wale ambao taarifa zao zitakuwa tayari katika bajeti 2021/22 itazingatia ili kulimaliza suala hilo.

Aliwataka watumishi kuwajibika wakati wakidai haki zao kwa kuwa hakuna haki bila wajibu.

Pia, alisema katika kuboresha uhusiano mzuri wa utendaji kazi serikali chini ya Rais Samia amesisitiza kufanya kazi kwa bidii na weledi ili kutoa huduma bora kwa Watanzania badala ya kutumia nguvu, ubabe na uonevu.

"Rais wetu msisitizo wake mkubwa ni katika kuwapigania watumishi wa umma na Watanzania wanyonge kwenye maeneo yao, kwa hiyo matumizi ya ubabe na uonevu si sehemu ya fikra za Rais wa awamu ya sita," alisema.

Alitoa wito kwa waajiri na watumishi wote kufuata maelekezo hayo kwamba matumizi ya mabavu na uonevu si sehemu ya fikra za rais.

"Tutafanya vizuri sana kama tutazingatia sheria katika masuala yote ya utawala bora, taifa letu lina uwezo wa kufanya vizuri sana kushinda wakati mwingine wowote, nasisitiza hilo, tunafanya hili ili wananchi wapate huduma bora bila kubugudhiwa," alisema.

Alihimiza waajiri wote kuhakikisha mabaraza ya wafanyakazi yanakuwa hai na kufanya kazi kikamilifu.

# Mlipuko wa baruti waua na kujeruhi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SONGWE

BARUTI zinazotumika kulipulia miamba kwenye machimbo ya dhahabu, zimelipuka ndani ya nyumba na kusababisha kifo cha mtu mmoja, majeruhi, kubomoa nyumba moja na zingine sita kuharibiwa vibaya.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, George Kyando, ambaye alifika eneo la tukio jana, alisema tukio hilo lilitokea juzi saa 10:00 jioni kwenye nyumba ya Daudi Mwakitalima iliyoko Mtaa wa Kigamboni, Kata ya Saza wilayani Songwe mkoani hapa.

Alimtaja mtu aliyefariki dunia kuwa ni Happymark Msuwila ambaye kutokana na mlipuko huo, viungo vya mwili wake kama mkono wa kushoto, figo na vipande vingine vya mwili vilikutwa nje kidogo na eneo kulipotokea mlipuko.

Kamanda Kyando alisema Msuwila alilipukiwa na baruti hiyo akiwa katika harakati za kuwapelekea wateja mzigo na kwamba aliyejeruhiwa amefahamika kwa jina la Jinasa Mayunga (54) ambaye baada ya tukio, alipelekwa katika Hospitali ya Misheni ya Mwambani ambako alitibiwa na kuruhusiwa.

Alisema katika tukio hilo, nyumba ya mwananchi huyo (Mwakitalima) imebomoka yote huku zingine sita za jirani zikipata madhara ya nyufa na madirisha kupasuka.

Kamanda Kyando alisema kutokana na tukio hilo, mmiliki wa nyumba iliyokuwa imehifadhi baruti hizo, anashikiliwa na polisi kwa tuhuma za kuendesha biashara haramu ya mlipuko. Pia ametoa siku mbili kwa wachimbaji madini ambao wanamiliki baruti au vilipuzi kinyume cha sheria, kuvisalimisha kwa ofisa madini na baada ya muda huo kwisha, kutafanyika msako na atakayekamatwa atachukuliwa hatua kali za kisheria.

# Makamba: Wanaoikosoa serikali wasiitwe wasaliti

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MBUNGE wa Bumbuli, January Makamba (CCM), amesema wanaoikosoa serikali, wakiwamo wabunge, wasichukuliwe kuwa ni wasaliti.

Alitoa kauli hiyo bungeni jana alipochangia mjadala wa mwelekeo wa kazi za serikali na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka ujao wa fedha.

Katika mchango wake, Makamba alianza kwa kutoa pole kwa Watanzania kwa kuondokewa na kiongozi wao aliyemwita jasiri na shupavu, Hayati Rais John Magufuli.

Aliwasilisha salamu za pole kwa familia ya Hayati Rais Magufuli, akisema kuwa msiba huo umeingiza nchi katika kipindi cha mpito ambacho hakikutarajiwa.

"Na mpito siku zote una mashaka, wasiwasi, hofu, mshtuko na huzuni. Kwa hiyo, wananchi kote nchi wana hayo mambo shaka, mshituko, huzuni na wasiwasi," alisema Makamba.

Alisema Rais mpya, Samia Suluhu Hassan, ametoa mwelekeo mpya ambao unaleta matumaini ya kuwapunguzia wananchi huzuni, shaka, mshtuko na wasiwasi.

Makamba alisema viongozi wote, wakiwamo wabunge, wanapaswa kujielekeza kwenye mwelekeo huo alioutoa Rais, akisisitiza kuwa kipindi ambacho nchi inahitaji umoja, utulivu na mshikamano ni sasa.

"Kauli za utengano, kauli za kutiliana shaka, kauli za kutuhumiana, hazijengi na zinawachanganya wananchi. Mambo makubwa aliyoyafanya Rais wetu aliyepita, Dk. John Pombe Magufuli hayatafutika, hayatafutwa, hayatapotea na hayatapotezwa kwa kauli yoyote ile.

"Hata hivyo, Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale miongoni mwetu ambao wanatoa maoni na ushauri wenye nia njema ya kuweka mambo sawa, ushauri wa kuyatengeneza vizuri, wasibezwe, wasihukumiwe katika dhamira zao.

"Dhamira ya kauli na ushauri na maoni ipo ndani ya moyo wa mtu. Mtu anaposifu kwamba Mama Samia ameanza vizuri, asihukumiwe kwamba anatafuta cheo, anapokosoa isionekane kwamba ana nongwa, anapokaa kimya isionekane kwamba amesusa.

"Ninaomba sana tusihukumiane katika dhamira za kauli zetu. Kazi aliyoifanya Rais Magufuli ninaichukulia kama ametushonea nguo nzuri kabisa ya kupendeza.

"Akitokea mtu akaona kwamba kwenye ile nguo kuna uzi umejitokeza tuukate, isionekane dhambi. Akipatikana mtu akasema kwamba katika hii nguo kifungo kimelegea tukiweke vizuri, isionekane mtu huyo ni msaliti.

"Na mtu huyo anapofanya kazi hiyo, tukikata kifungo, tukikaza uzi, nguo ikapendeza, bado sifa ni ya mshonaji. Mimi ninaomba sana kwa sababu dalili nilizoziona siyo nzuri sana.

"Sisi kama viongozi, tunao wajibu wa kutoa maoni kuhusu mambo yetu yaendeje, lakini njama, vikundi, magenge ya kuweka mashinikizo kwamba kipi kifanyike, kipi kichukuliwe, kisichukuliwe si sawa kabisa na haitujengei umoja."

Makamba alisema Rais wa nchi ana madaraka makubwa na kila Rais aliyeongoza Tanzania ameacha alama na kwamba wajibu wa viongozi waliopo ni kuyalinda mema yaliyofanywa na watangulizi wao.

"Kwa hiyo, sisi tupiganie kuyalinda mema yaliyofanywa na Rais Magufuli lakini tusipigane wakati tunafanya hivyo. Tukipigana kwa mambo ya nyuma, tutashindwa kupigania mambo mazuri ya mbele ambayo Rais mpya anataka kuyafanya.

"Vikumbo vya nani ni mnazi zaidi wa Rais Magufuli, nani ni mnazi zaidi wa Rais Samia na viwiko vikali zaidi ambavyo watu wanataka kupigana, havisaidii wala havijengi.

"Tuheshimiane, tusihukumiane na tumsaidie kiongozi wetu, tuwe na umoja, utulivu kwa sababu utulivu ndani ya Bunge ndiyo utasaidia kiongozi wetu kutawala vizuri," alihitimisha.

## HABARI KITAIFA

# Mtoto wa shule darasa la nne ajinyonga hadi kufa

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

MWANAFUNZI wa darasa la nne Shule ya Msingi Muungano, wilayani Tunduru, mkoani Ruvuma, Abdul Abubakar (12), amejinyonga hadi kufa.

Taarifa zinazeleza kuwa mwanafunzi huyo alijinyonga kwa kutumia shuka Aprili 11, mwaka huu majira ya saa saba mchana baada ya kuwaaga wazazi wake kuwa anaenda kuangalia tamthilia akiwa anasubiri chakula cha mchana.

Akizungumzia tukio hilo, baba mzazi wa marehemu Abubakar Kazembe, alisema siku ya tukio alikuwa na mtoto wake na alimtuma kwenda sokoni, aliporudi walikaa pamoja wakiwa wanasubiri chakula na alishtushwa kupata taarifa kuwa mwanawe amefariki dunia kwa tukio hilo.

Kazembe alisema wakati wanasubiri chakula, yeye na mama yake walianza kumtafuta bila mafanikio na walipo ingia chumbani kwake walimkuta akiwa ananing'inia juu ya paa la chumba.

Mganga aliyeufanyia uchunguzi mwili wa marehemu Abdul, Dk. Athuman Mkono, alithibitisha kuwa chanzo cha kifo hicho kilitokana na tendo la kujibana mishipa ya shingo na kukosa hewa.

Akizungumzia tukio hilo Kaimu Kamanda wa Mkoa wa Ruvuma Kamishna Msaidizi wa Polisi, Amini Mahamba, alisema wanaendelea na uchunguzi wa chanzo cha tukio hilo.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akitembelea jengo jipya la abiria la Terminal 3 katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume Zanzibar jana. Kulia ni Msimamizi wa Ujenzi wa jengo hilo, Mhandisi Yassir De Coster. **PICHA: IKULU**

# Waliofariki dunia Same wafikia 11

**Na Mary Mosha,** MOSHI

IDADI ya watu waliofariki dunia katika ajali ya gari iliyohusisha basi dogo la abiria aina ya Toyota Hiace na Toyota Alphard, imefikia 11, huku majeruhi sita ambao hali zao ni mbaya, wakihamishiwa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, alithibitisha waliofariki dunia katika ajali hiyo kuongezeka usiku wa manane.

Mghwira alitoa taarifa hiyo jana baada ya kwenda KCMC kuwajulia hali majeruhi waliolazwa wodi ya wagonjwa walio katika uangalizi maalum (ICU).

Akizungumzia ajali hiyo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Amon Kakwale, aliwataja waliofariki dunia kuwa ni Juma Msuya, Adam Msuya, Mwajuma Haji (70), Nietiwe Hemed (47), Ngai Walter, Amon John na Samwel Julius Mbaga (44).

Kamanda Kamwale alisema watu hao walipoteza maisha baada ya gari aina ya Toyota Alphard lenye namba T 898 DKX lililokuwa likitokea Arusha kwenda Lushoto mkoani Tanga, kupasuka tairi la nyuma la upande wa kushoto na kupoteza mwelekeo, hivyo kusababisha kugongana uso kwa uso na basi dogo la abiria lenye namba T 806 BNM.

Alisema ajali hiyo ilitokea katika Kijiji cha Kirinjiko, wilaya ya Same. Basi dogo la abiria (Hiace) lenyewe lilikuwa likitokea Hedaru kwenda Same.

"Alphard ilipata 'tyre bust' (kupasuka gurudumu) ya nyuma ikayumba ikaenda kugongana na hiyo Hiace. Katika Hospitali ya Wilaya ya Same wamebaki watu wanne ambao wanaendelea kupatiwa matibabu na sita wamekimbizwa Hospitali ya Rufani ya KCMC.

"Aidha, miili minne imetambuliwa na sita ndugu zao walikuwa wanaendelea kutafutwa," alisema.

Akiwa KCMC, Dk. Mghwira alisema: "Leo (jana) nimetembelea majeruhi sita waliopata ajali kule Same, watatu kati yao, licha ya kwamba nimeambiwa wanaendelea vyema. Lakini kwa mwonekano wanapumua kwa shida, yaani kwa ujumla hali zao si nzuri."

"Nimepokea taarifa za madaktari, wanasema watu hao wameumia kwenye maeneo ya kichwa na kuvunjika mifupa mikubwa ya miguu. Nitoe wito kwa Jeshi la Polisi, hasa Kikosi cha Usalama Barabarani kupanga ukaguzi wa magari haya mara kwa mara ili kuepusha hiki kinachowagharimu wenzetu," aliongeza.

Akitoa taarifa ya maendeleo ya wagonjwa hao, Daktari Bingwa wa Mifupa, Mugisha Nkoronko, alisema majeruhi waliopokelewa katika wodi namba sita ni wawili.

Alisema mgonjwa mmoja amepata majeraha katika kichwa na yameathiri sana mfumo wa kuongea na mwingine amevunjika mfupa mkubwa wa paja na anaendelea na matibabu.


AccessBank
TANZANIA • ACCESS GROUP

**TAARIFA KWA UMMA**

**MABADILIKO YA JINA NA AINA YA LESENI YA KIBENKI**

**Dar es Salaam, 15 April 2021**

AccessBank Tanzania Limited (ABT) inayo furaha kutangaza mabadiliko yake kutoka Leseni ya Benki ya Biashara kwenda Leseni ya Benki ya Microfinance, na hivyo kubadilisha jina lake kuwa Access Microfinance Bank Tanzania Limited (AMBT). Mabadiliko haya ya leseni yameidhinishwa na Benki Kuu ya Tanzania kuanzia tarehe 01 Machi 2021.

ABT imekuwa ikiendesha shughuli za kibenki tangu 2007, ikifanya kazi kwa leseni ya benki ya kibiashara kama ilivyotolewa na Benki Kuu ya Tanzania. Tangu kuanzishwa kwake, imetoa zaidi ya mikopo takribani 236,000 yenye thamani ya Shilingi za Kitanzania 1,300Bilioni.

ABT inamilikiwa na wanahisa watano mashuhuri wa kimataifa ambao ni Access Microfinance Holding AG (AccessHolding) iliyoko Ujerumani, Shirika la Benki ya Dunia linalojishugulisha na sekta binafsi linaloitwa 'International Finance Corporation', ambayo ni sekta ya sekta binafsi ya Benki ya Dunia, Micro Vest, kikundi cha kibinafsi cha uwekezaji wa faida huko Marekani, KfW - Benki ya Maendeleo ya Ujerumani inayomilikiwa na Jamhuri ya Shirikisho la Ujerumani na majimbo yake ya Shirikisho, na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ambayo ni taasisi ya kifedha ya maendeleo ya nchi nyingi za Kiafrika. Pamoja na badiliko la jina hakuna mabadiliko ya wanahisa.

Mabadiliko haya yanaonyesha mwelekeo wetu wa kina kwa wateja wetu wote kuanzia wadogo na wakati, ambao tayari wanachangia takribani asilimia tisini na tano (95%) ya jumla ya idadi ya mikopo yote iliyotolewa. AMBT itaendelea kuwa benki ya kipekee kwa wafanya biashara ndogo ndogo na za kati pamoja na kuwa benki inayowajibika kwa jamii. Wigo wa huduma zetu na bidhaa utabaki bila kubadilika na tutaendelea kuhudumia jamii nzima. Access Microfinance Bank Tanzania Limited kama ilivyokuwa kwa AccessBank Tanzania Limited itaendelea kufuata taratibu, sheria na miongozo ya Benki Kuu ya Tanzania kwa mujibu wa sheria.

Access Microfinance Bank Tanzania Limited itaendelea kusimamia dhamira na maono yale yale ya AccessBank Tanzania Limited, ikifanyia kazi katika matawi yale yale, ikiendelea kuwahudumia wadau wote kwa ufanisi na umakini zaidi. Tunaishukuru sana Benki Kuu ya Tanzania kwa ushirikiano na miongozo sawia. Pia tunathamini sana juhudi na utendaji bora wa wafanyakazi , na uaminifu wa maelfu ya wateja wetu.

Kwa mujibu wa sheria za nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zinaweka wazi na kwa usahihi kuwa, mabadiliko haya hayataathiri haki au wajibu wowote wa benki au kutoa madai / mwenendo wa kesi yoyote ya kisheria, wala kuathiri maslahi au utekelezaji wowote wa madai au kesi zozote, hivyo kila kitu kitahama kutoka AccessBank Tanzania Limited kwenda Access Microfinance Bank Tanzania Limited.

AMBT inaendelea kutekeleza hatua mbalimbali za uboreshaji wa utendaji ambazo zinaonyesha matokeo mazuri, kwani benki sasa iko katika kufikia utendaji endelevu wa kuridhisha.

Kama zilivyo benki nyingine, AMBT inaendelea kuendeshwa na kusimamiwa kwa kanuni za Benki Kuu ya Tanzania.

Kwa maswali zaidi, tafadhali usisite kuwasiliana nasi kupitia kitengo chetu cha huduma kwa wateja kwa namba zifuatazo +255 659 074000 na +255 784 108500 au kupitia barua pepe customersupport@accessbank.co.tz

**Imetolewa na;**
**Bodi ya Wakurugenzi wa Access Microfinance Bank Tanzania Limited.**

MAHOJIANO MAALUM:

# Msekwa afunguka kuhusu Samia

**Na Romana Mallya**

SPIKA wa Bunge mstaafu, Pius Msekwa (pichani), amefunguka na kueleza kuwa hana wasiwasi na mwelekeo wa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa sababu ya uwezo na uzoefu wake wa kufanya kazi Ikulu.

Katika mahojiano maalum na Nipashe, Spika huyo mstaafu na mwanasiasa nguli aliyehudumu serikalini kwa kushika nyadhifa mbalimbali, anasema Rais Samia anabebwa na tabia yake, uzoefu, kazi alizozifanya ambazo zilimwezesha kuteuliwa kugombea nafasi ya Makamu wa Rais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Samia aliapishwa rasmi Machi 19, mwaka huu, kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kifo cha mtangulizi wake Hayati John Magufuli, aliyefariki dunia Machi 17.

Madaraka hayo yanamfanya kuwa mwanamke wa kwanza ukanda wa Afrika Mashariki kushika wadhifa wa juu wa urais baada ya kuhudumu katika nafasi ya Makamu wa Rais kwa miaka mitano na miezi mitano.

Akimzungumzia Rais Samia, Msekwa anasema amefurahishwa na mwelekeo wake.

"Nimefurahia sana mwelekeo wa Rais tuliyenaye sasa, kwa upande wangu nilipata bahati ya kumfahamu vizuri kabla hajaingia Ikulu hata katika nafasi yake ya Makamu wa Rais.

"Nilipata bahati hiyo ndani ya CCM, tuna Baraza la Wazee la Ushauri linaloundwa na waliokuwa wenyeviti wa chama yaani Marais na Makamu Wenyeviti. Binafsi niliwahi kuwa Makamu Mwenyekiti CCM wakati wa uenyekiti wa Rais mstaafu Jakaya Kikwete, nipo ndani ya baraza hilo na mimi ndiye Katibu wa Baraza kwa sasa," anasema.

Inapofikia hatua ya kupendekeza mgombea Urais na Makamu wa Rais wa CCM, baraza hilo hushirikishwa.

"Mwaka 2015, katika Uchaguzi Mkuu, tulishirikishwa ndipo nikapata bahati ya kumfahamu Samia, kwa sababu katika kumpitisha mgombea mnaangalia kazi zake za nyuma, uzoefu wake, tabia zake za nyuma na yanaangaliwa mambo mengi na yote yanawekwa mbele ya baraza, nikapata bahati ya kumfahamu vizuri.

"Nina imani naye kama waliyonao watu wengine kwamba tumepata rais atakayeendeleza pale Hayati Rais John Magufuli ameachia," alisema.

Kuhusu ushauri wake kwa Rais Samia, alisema hadhani kama anauhitaji kwa sababu tayari ni mzoefu wa kazi za urais iliyotokana na ukaribu wake na Hayati Magufuli.

"Hiyo peke yake ni sifa kubwa kwamba hajaingia kutoka nje, ni mtu wa ndani ya Ikulu, sidhani kama anahitaji ushauri, tulichokiona ni utendaji wake ambao unaonekana kupitia kauli zake anazozitoa anapowaapisha aliowateua.

"Kwanza, uteuzi wake wa Baraza la Mawaziri, niliona kitendo chake cha kubaki na mawaziri wote walioteuliwa na Rais Magufuli, kwamba ana lengo la kuendeleza juhudi zilezile za Hayati Magufuli, ndiyo maana akabaki na timu ile ile ili kusiwe na mabadiliko makubwa ya ghafla ghafla."

**UTEUZI MAKATIBU WAKUU**

Kuhusu uteuzi alioufanya hivi karibuni wa Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na wakuu wa taasisi na idara mbalimbali alioufanya Aprili 4, anasema Rais Samia ameonyesha mwelekeo mwingine kwamba pamoja na kuendeleza ya mtangulizi wake, ana ya kwake ambayo atayasimamia mwenyewe na timu anayoiunda.

"Alipokuja kuteua Makatibu Wakuu, alikuwa ni yeye mwenyewe, ni kama mtu aliyekwenda baharini katika bahari kubwa la utumishi wa serikali akavua samaki wake wenyewe."

**NYAYO ZA MAGUFULI**

Maelekezo ya Rais Samia dhidi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), anasema yanaonyesha kwamba anataka kuendeleza msimamo wa Hayati Magufuli kwa kutegemea mapato ya ndani kwa kiasi kikubwa katika kuendesha shughuli za serikali huku akisifu kuwa jambo hilo ni muhimu.

"Mwanzo wake, ameshatuonyesha mwelekeo wake, na ukitizama maelekezo aliyoyatoa kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana Rushwa (TAKUKURU) kupitia taarifa alizozipokea kuhusu fedha nyingi zilichotwa kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT), akaagiza uchunguzi ufanywe, hii peke yake vilevile inaonyesha kwamba yupo makini kupambana na ubadhirifu wa fedha za umma kwa matumizi yasiyofaa."

Msekwa anasema Rais Samia chini ya mwezi mmoja ameonyesha mengi na anaungana na Watanzania kutamka kwamba, "Nina imani na uwezo wake kushika nafasi hii, atatuongoza vizuri katika muda wake wa kumalizia kipindi hiki na pale atakapoanza kipindi chake mwenyewe katika uchaguzi utakaofuata," anasema.

**TAALUMA ZA WATEULE**

Anasema kitendo cha Rais kupanga safu yake kwa kuzingatia taaluma ni jambo la muhimu kwa sababu watu wanatakiwa kufanya kazi kulingana na ujuzi walionao.

"Kiongozi yafaa awe na ujuzi wa kazi anayoifanya, vinginevyo kama hana basi awe ni mtu mwenye uwezo wa kufanya jitihada za kuelewa majukumu aliyopewa haraka haraka, hii ndiyo ishara aliyotupatia katika uteuzi wake alioufanya hivi karibuni.



"Anataka kuweka watu wenye ujuzi kwenye nafasi za uongozi ambayo inasaidia sana kupeleka gurudumu la maendeleo mbele kwa sababu ujuzi ni madaraka, ukishakuwa na ujuzi tayari una madaraka ya kutekeleza mambo vizuri sana."

**UTAWALA BORA**

Anasema Rais Samia amewapa mwelekeo mzuri wa kusimamia utawala bora, haki za binadamu na demokrasia baada ya hotuba zake kukemea tabia ya baadhi ya viongozi.

"Kule kukemea kwake kunaonyesha kwamba anataka kuona wasaidizi wake wanaendesha serikali kwa mujibu wa utawala bora na utawala unaofuata sheria."

Kuhusu athari za kuendesha serikali kwa utawala wa mtu mmoja badala wa sheria, Msekwa anasema bado hajauona na kueleza kuwa hizo ni hisia za baadhi ya watu.

"Katika mfumo wetu haiwezekani kuwa na utawala wa mtu mmoja, Katiba imeweka mfumo lazima kiongozi wa nchi atawale kwa pamoja, ndio maana limewekwa Baraza la Mawaziri ambalo kwa mujibu wa Katiba ndilo linalomshauri.

"Uongozi wa mtu mmoja ni kukiuka Katiba ambayo mimi dalili hizo zijaziona katika marais wetu," anasema.

**KATIBA MPYA**

Anasema Katiba Mpya ni matamanio ya kundi la watu na sio wote wanayoitaka kwa sababu tayari nchi inayo na wanayoyasema kama upungufu, kwake hayaingii akilini.

"Kwa mfano wanasema Katiba haijaweka Tume Huru...Tume Huru haiwekwi na Katiba, uhuru wa tume unategemea waliopewa kazi hiyo, uhuru wa kuiongoza unategemea namna anavyoifanya kazi yake si Katiba.

"Katiba nyingi zinatamka hivyo, Katiba huru ya Kenya, tume huru ya uchaguzi Kenya, tume huru ya uchaguzi ya Afrika Kusini, ni maneno tu ya kwenye maandishi, lakini uhuru wa tume hautokani na maandishi, unatokana na vitendo vya wanatume wenyewe, kwahiyo mambo kama hayo hayaingii akilini, hayana mvuto mkubwa, haya ni maoni yangu."

**MWENYEKITI CCM**

Akimzungumzia Rais Samia katika nafasi ya Mwenyekiti wa CCM Taifa na mabadiliko ndani ya chama, Msekwa anasema kubadilisha chombo ambacho kiongozi mpya anaingia, kunategemea na mtazamo na mwekeleo wa mhusika.

"Anataka mambo yaende vipi, huwezi kubashiri mapema, huwezi kupiga ramli, ukasema atabadilisha. Ninavyoona sasa hivi CCM inakwenda vizuri, tuliisuka tangu tulivyokuwamo, nikiwa Katibu Mkuu Mtendaji wa CCM na mwanzilishi haswaa, CCM tuliisuka vizuri na Mwalimu Julius Nyerere (Baba wa Taifa).

"Tuliisuka kimfumo, kitaratibu, kikanuni, kwa hiyo kukosoa mfumo uliopo umeendelea hivyo hivyo tangu mwaka 1977 hadi leo, kufumua kutokana na upungufu ni ngumu, kitu kilichosukwa vizuri kikafanya kazi kwa muda wote huo, sana sana atabadilisha watu wa kuendesha, ambao lazima wabadilike kwa sababu kuna uchaguzi kila baada ya miaka mitano.

**Itaendelea kesho**

TANGAZO

# YETU MICROFINANCE BANK PLC

Yetu Microfinance Bank PLC
"Creating Wealth Together, Pamoja Tunaweza"

## Taarifa za fedha kwa umma zilizokaguliwa kwa Mwaka ulioishia Tarehe 31 DISEMBA 2020

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DISEMBA 2020.
Kiwango kwa Tzs.'(000)'

| | | Mwaka wa sasa 31-Dec-20 TZS | Mwaka Uliopita 31-Dec-19 TZS |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 1,209,570 | 352,173 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 229,958 | 268,200 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | | 0.00 |
| 4 | Salio katika Benki Nyinginezo na Taasisi za Fedha | 102,062 | 1,331,810 |
| 5 | Hundi na Miamala ya kushughulikiwa | | |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | | |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | | |
| 8 | Dhima za Wateja zilizokubalika | | |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki Nyingine | | |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | | |
| 11 | Mikopo Halisi iliyopo | 15,449,608 | 15,710,854 |
| 12 | Mali Nyingine | 859,333 | 824,772 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | | |
| 14 | Limbikizo la Mali Kodi | 701,445 | 442,003 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | **952,051** | 650,144 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | 19,504,027 | **19,579,956** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | | |
| 18 | Amana za Wateja | **2,246,776** | **2,123,472** |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | | |
| 20 | Amana Maalumu | **1,517,501** | **2,017,237** |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | | |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | | |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | | **7,165** |
| 24 | Dhima la Tozo kwa ajili ya usuluhishi baina ya Benki na Mteja | | |
| 25 | Mtaji wa Wahisani | | **64,446** |
| 26 | Mapato yalioingia ya kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa baadae | | |
| 27 | Dhima Nyingine | **176,774** | **409,097** |
| 28 | Madeni | **7,000,000** | **6,500,000** |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **10,941,052** | **11,121,417** |
| 30 | **MALI/{DHIMA} HALISI** | **8,562,976** | **8,458,539** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | **6,056,497** | **6,056,497** |
| 32 | Akiba ya Mtaji | | |
| 33 | Mapato yaliyobakizwa | 2,439,474 | **1,650,972** |
| 34 | Faida/{Hasara} ya Kipindi Husika | - | **681,377** |
| 35 | Akaunti zingine za Mtaji | 67,005 | **69,693** |
| 36 | Stahiki ya wenye Hisa chache | | |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | 8,562,976 | **8,458,539** |
| 38 | Dhima zisizo dhahiri | **0** | |
| 39 | Mikopo chechefu | **1,244,182** | **892,734** |
| 40 | Tengo Kwa ajili ya mikopo chechefu | **1,184,439** | **1,033,270** |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | | |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | **%** | **%** |
| i | Uwiano wa Fedha za wanahisa na Jumla ya Mali | 44% | 43% |
| ii | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 7% | 5% |
| iii | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | **442%** | **404%** |
| iv | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 79% | 80% |
| v | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 79% | 80% |
| vi | Ongezeko la Amana | **0%** | 85% |
| vii | Ongezeko la Mali | **0%** | **31%** |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DISEMBA 2020.
Kiwango kwa Tzs.'(000)'

| | | Mwaka wa sasa 31-Dec-20 TZS | Mwaka Uliopita 31-Dec-19 TZS |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 4,013,146 | 4,969,115 |
| 2 | Gharama za Riba | 800,676 | 586,723 |
| **3** | **Mapato Halisi (1 kutoa 2)** | **3,212,470** | **4,382,392** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | | |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika mikopo | 53,204 | 196,143 |
| **6** | **Mapato yasiyo ya Riba:** | **700,746** | **695,686** |
| | | 0 | |
| | 6.1 Faida/(Hasara) zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | | |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 539,365 | 588,483 |
| | 6.3 Gawio | | 0 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 161,381 | 107,202.41 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **4,174,438** | **4,478,061** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 2,279,724 | 2,344,063 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 30,000 | 0 |
| | 7.3 Gharama nyingine | 1,864,714 | 2,133,999 |
| 8 | **Faida/(Hasara) ya Uendeshaji** | **(314,425)** | **796,159** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (259,442) | 114,782 |
| 10 | **Faida/(Hasara ) Halisi baada ya Kodi ya Mapato** | **(54,983)** | **681,377** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa{bainisha} | **0.00** | **0.00** |
| 12 | **Jumla ya Faida/{Hasara} iliyojumuishwa kwa Mwaka** | **(54,983)** | **681,377** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | **125** | 134 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | - **0.45** | 56 |
| 15 | Idadi ya Matawi | **3** | 3 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (i) | Uwiano wa Faida kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | **22%** | 22.38% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | **52%** | 51.81% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | **102%** | 102.18% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | **28%** | 27.89% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DISEMBA 2020
Kiwango kwa Tzs '(000)'

| | | Mwaka wa sasa 31-Dec-20 TZS | Mwaka Uliopitia 31-Dec-19 TZS |
|---|---|---|---|
| **I** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **(314,385)** | **796,159** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | | |
| | - Faida/{Hasara} kwenye Mauzo ya Mali | **442,003** | - |
| | -Uchakavu wa Mali za Kudumu | **230,534** | 213,125 |
| | -Uchakavu wa Matengenezo Makubwa | | |
| | -Utumikaji wa Mtaji wa Misaada | **-** | - |
| | -Uchakavu wa Mali Zisizoshikika | | |
| | | **358,152** | **1,009,285** |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Salio la Benki Kuu ya Tanzania | **-** | - |
| | - Badiliko Halisi katika Mikopo | **261,246** | (3,096,926) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | **-34,561** | 48,488 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | **(376,431)** | 1,907,794 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika salio la benki Nyingine na Taasisi za Fedha | **-** | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | **-232,323** | (484,274) |
| | | **(23,917)** | **(615,634)** |
| | - Kodi Iliyolipwa | **(150,000)** | (174,000) |
| | Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji | **(173,917)** | **(789,634)** |
| **II** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| | Gawio Lililopokewa | | |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | **(331,155)** | (422,386) |
| | Mapato kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | | |
| | Ununuzi wa Mali Zisizoshikika | **(201,288)** | |
| | Mengineyo Amana za kudumu | | |
| | Mapato kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | | |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa** | **(532,443)** | **(422,386)** |
| **III** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | **-** | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | **500,000** | 2,500,000 |
| | Mtaji Kutokana na Utoaji wa Wahisani | **68,319** | 64446.00 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | | |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | **(272,551)** | (424,817) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | **-** | - |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha* | **295,768** | **2,139,629** |
| **IV** | **Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| | Ongezeko/ Punguzo Halisi katika Fedha taslimu na Mali zinazofanana na Fedha | **(410,592)** | **927,609** |
| | Fedha na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | **1,952,182** | 1,024,573 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka | **1,541,590** | **1,952,182** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DISEMBA 2020

| Kiwango kwa Tzs.'(000)' | Mtaji wa Hisa | Mtaji mkuu wa kisheria | Mtaji wa kisheria | | Akaunti zingine za Mtaji | Tengo la ziada ya jumla | Jumla Tzs |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la wa mwaka 01/01/2019** | **6,056,497** | **130,555** | **-** | | **69,693** | **1,511,458** | **7,768,203** |
| Rekebisho : | | | | | | | - |
| Ongeza: Jumlisha/(Futa) kwa kipindi cha mwaka | - | - | - | | - | - | - |
| Toa: Mapato mengine | - | (130,555) | - | | - | 130,555 | - |
| Mtaji mkuu wa kisheria | | - | - | | | - | - |
| Mtaji wa kisheria | | | - | | | 433,776 | 433,776 |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya kodi ya mapato | - | - | - | | - | 681,377 | 681,377 |
| Gawio lililolipwa | | | | | | (424,817) | (424,817) |
| **!"#$%&'("&)(""&*+,+-,-.+/** | **6,056,497** | **-** | **-** | **-** | **69,693** | **2,332,349** | **8,458,539** |
| **Salio la mwaka 01.01.2020** | **6,056,497** | **-** | **-** | | **69,693** | **2,332,349** | **8,458,539** |
| Rekebisho : | - | | | | | | - |
| Toa: Mapato mengine | - | - | | | (69,693) | 67,006 | (2,687) |
| Limbikizo la mali mtaji kwa mwaka Jana | | | | | - | 434,618 | 434,618 |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya kodi ya mapato | - | | | | | (54,944) | (54,944) |
| Toa: Gawio lililotolewa | - | | | | | (272,551) | (272,551) |
| **!"#$%&'("&)(""&*+,+-,-.-.** | **6,056,497** | **-** | **-** | | **-** | **2,506,478** | **8,562,975** |

### ADA NA GHARAMA ZA HUDUMA KWA MWAKA ULIOISHIA 31.12.2020

| 1. AKAUNTI ZA AKIBA | | | 2. Mkopo | |
|---|---|---|---|---|
| Kima cha chini cha kufungu | 5000/= | | Mikopo ya biashara | 36% PA |
| Ada ya mwezi | BURE | | Mikopo ya kuboresha nyu | 18% PA |
| Taarifa ya Akaunti | BURE | | Ada ya Mkopo | 2.5% |
| Kuuliza salio | BURE | | Bima ya mkopo | 2% |
| Kufunga akaunti | 5000/= | | Mkop wa Pembejeo | 30% PA |
| Gharama za kuendesha akau | 5000/= | | Mkopo wa Kilimo | 30% PA |
| Gharama za kuweka fedha | BURE | | Mikopo ya Staff | 15% PA |
| Account maintanance charg | FREE | | Mikopo ya Maji | 26% PA |
| Account maintanance charg | FREE | | | |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, Taarifa za fedha zimekaguliwa na HLB MEKONSULT na kutoa Hati safi.

**Kuthibitishwa na:**

*Ernest K. Ndimbo* *Mwenyekiti wa Bodi* .............................. *08.04.2021*

*Cornelius Kariwa* *Mkurugenzi* .............................. *08.04.2021*

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mapitio kanuni kikokotoo kipya yawe mwarobaini

**JUZI** Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alieleza bungeni nia ya serikali kushirikisha wadau katika kutoa maoni yao kwenye mapitio ya kanuni za utekelezaji wa sheria ya Mfuko wa PSSSF ya mwaka 2018.

Baada ya Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa umma namba 2 ya mwaka 2018 kupitishwa na Bunge januari 31, mwaka 2018, iliunganisha mifuko minne ya pensheni ya PSPF, PPF, GEPF na LAPF. Sheria ya PSSSF ilisainiwa Februari 8, mwaka 2018 na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Februari 9, mwaka 2018 na imegawanyika katika sehemu 11.

Aidha, kanuni za utekelezaji wa sheria ya PSSSF zilikamilishwa na kutangazwa katika gazeti la serikali.

Sheria hiyo ambayo imeweka jumla ya mafao manane; pensheni ya uzeeni, pensheni iliyohairishwa, fao la ulemavu, fao la warithi, fao la upotevu wa ajira, fao la ugonjwa, mkopo wa nyumba na fao la uzazi, ambayo yote yameainishwa jinsi yatakavyotekelezwa kwenye kanuni hiyo. Mjadala huo ulianza baada ya iliyokuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Hifadhi ya Jamii (SSRA), kutoa elimu ya kanuni hizo, ambazo zilibeba fomula itakayotumika kwenye kikokotoo.

Kwenye kanuni hizo kikokotoo ili kupata malipo ya mkupuo (fedha anayoipata mstafu mara baada ya kustaafu) kilitofautiana kwa kila mfuko. Kwa PSPF kilikuwa ni mshahara wa mwezi, kiwango cha uchangiaji, muda wa uchangiaji na jumla ya michango ndipo mtu anapata malipo ya mkupuo wa asilimia 50 na kiasi kinachobakia kinalipwa kila mwezi.

Kwa kikokotoo cha zamani mtu alipata kwa mkupuo fedha nyingi na kila mwezi alipata fedha kidogo kulingana na kiwango cha uchangiaji wake, na ndiyo sababu ya wadau kuibua malalamiko kwa kuwa hawakukubali kupunguziwa mafao ya mkupuo na kuongezewa pensheni ya kila mwezi.

Kwa kikokotoo kipya mtumishi analipwa asilimia 25 ya fedha za mkupuo, huku pensheni ya kila mwezi ikiwa kubwa ambayo inamwezesha mstaafu kuishi na muda wa kuishi kwa vikokotoo vyote ni miaka 15.5. Baada ya kilio cha wadau kuwa kikubwa, Rais Hayati Dk. John Magufuli, alitangaza kusitisha matumizi ya kikokotoo kipya hadi 2023, ndipo mchakato utaanza upya.

Sasa Waziri Mkuu anatoa mwelekeo mpya wa kuwa wadau watashirikishwa kwenye kanuni za sheria hiyo, hii inaonyesha kuwa pamoja na uwapo wa kanuni ya sheria hiyo, sasa yatafanyika mapitio na kushirikisha wadau ipasavyo.

Tunatambua kuwa awali wakati wa mchakato wa sheria hii hadi kupata kanuni yake, wadau walishirikishwa, na sasa watashirikishwa tena. Ni muhimu kuhakikisha suala hilo linatangazwa vyema kwenye vyombo vya habari, mitandao ya kijamii na namna rasmi ya mawasiliano serikalini ili kuwafikia wadau wote, ili kusiwe na msuguano mwingine kanuni mpya zitakapoanza kazi.

Kilio kikubwa cha waajiriwa hasa wa umma ni kukubali kikokotoo kipya, ambacho kinaelekeza malipo ya mkupuo kuwa asilimia 25 badala ya 50 ya awali.

Kwa wanachama wa NSSF, ambao ni wa sekta binafsi kikokotoo chao ni asilimia 25, na wameishi hivyo kwa miaka yote. Iliyokuwa SSRA ilisema lengo la kuja na kikokotoo hicho ni kuiokoa mifuko ya umma ambayo kwa wakati huo mingi ilikuwa taabani kiasi cha kushindwa kulipa mafao kwa wakati, na ikiwa italipa mafao kama NSSF maana yake itaweza kujiendesha kwa muda mrefu.

Lakini wadau walipinga kwa kuwa walishaweka malengo ya kupata malipo mengi ya mkupuo na kidogo kila mwezi, huku wengine wakiwa hawana uhakika wa maisha kwa muda mrefu baada ya kustaafu. Tunatarajia kuwa mapitio ya kanuni hizo utakuwa ni mwarobaini kwa wadau wote hususani watumishi wa umma, ambao kikokotoo kipya wataanza kukiishi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kuoshana maji machafu, matope, vyakula 'sakafuni' Mabibo sokoni

Na Yasmine Protace

NIANZE kwa kusema katika maisha ya kawaida iwe mijini na hata vijijini, sokoni ni mahali muhimu tunakoweza kupata bidhaa mbalimbali na kwa namna ya kipekee vyakula, ili kukidhi mahitaji yetu ya kila siku.

Hata zaidi ya hapo, mengine mengi ya dukani nayo yapo. Vivyo hivyo, ikiangaliwa upande mwingine ambako nako bidhaa zote zinauzwa mahali hapo.

Ni kivuli kimoja muhimu kilichoko sasa kwamba, wanaofanya biashara katika soko la Mabibo, hivi sasa wanatakiwa kujali afya za walaji matunda na bidhaa nyinginezo, huku serikali na mamlaka nyinginezo nazo zinapatumia kukusanya haki zao.

Hapo ndipo simulizi yangu inakuja katika dhana kile ninachokishuhudia katika Soko la Mabibo, lililoko jijini Dar es Salaam na pengine masoko mengineyo, mvua hizo za msimu zikiendelea.

Hapo Mabibo, maarufu kwa jina la 'Soko la Ndizi' mti anapokuwa mahali hapo, hali ya uchafuzi wa afya na mazingira imetawala kila mahali.

Ni daima kuna biashara za matunda mbalimbali, viazi mikungu ya ndizi, nyanya, viazi vya aina yote, mihogo vilivyopangwa chini vinauzwa. Niseme ni tabia endelevu ambayo haipendezi hata kidogo!

Hapo, muhimu kinachotakiwa mahali hapo ni suala la kujali afya za walaji na bidhaa hizo kupangwa katika maeneo safi na salama.

Inapofika kipindi cha mvua, ndipo mtu anaweza kushuhudia uwapo wa baadhi ya wafanyabiashara wanaopanga matunda na bidhaa zingine katika maeneo yasiyofaa kiafya.

Mtu anakuta matope mahali hapo, matunda yamepangwa chini na hakuna wanachojali hata kidogo. Kuna baadhi ya maeneo ya kibiashara mahali hapo, wafanyabiashara wanauza mikungu ya ndizi wanayoiweka sehemu isiyo rafiki kwa afya ya mlaji.

Unakuta mikungu inaangukia katika matope ambayo kupitia angalizo la jicho pekee, inahatarisha afya ya mlaji.

Kuna uhalisia wa mtu anapofika eneo la Kituo Cha Mafuta Cha Kona, kuelekea Mabibo Sokoni, kuna ushuhuda wa biashara za mboga za majani, dagaa, nyanya na tangawizi zilizowekwa chini ukanda wenye matope na uchafu inakotoa maji yenye harufu na yametuama.

Sambamba na hiyo, nimeshuhudia madimbwi ya maji machafu, hata kuwa kikwazo kwa wapita njia, wanatumia mbadala wa kupanda mawe, ili kupita na kupelekwa sehemu nyingine.

Sasa kinachoshangaza, ni pamoja na kuwapo maji hayo, bado biashara za mboga zinaendelea. Ni dhahiri afya za walaji ziko hatarini.

Pia, mtu akisogea katika geti la kuingilia sokoni, ni mahali penye mtaro unaomwaga maji machafu. Hapo kuna vijana ambao wamejikita katika jukumu la aina yake, wanatumia maji hayo kuosha mifuko na kwenda kuiuza.

Kimsingi, ni mambo ambayo hata hayajulikani yalikotoka, lakini vijana wa sokoni wanachukua mifuko hiyo wanaiosha na kwenda kuiuza na wanapata wateja.

Kutokana na kipindi kilichopo kuwa cha mvua kunyesha, wapo watu wanaotafuta riziki katika soko hilo kwa kuwauzia kofia kinamama nywele zao zisilowe.

Pia, wapo wanaoosha watu miguu, kutokana na matope, wengine wanakodisha buti kwa waingiaji sokoni.

Sasa, ukiangalia wale wanaokodisha mabuti ili watu waingie sokoni, ni viatu ambayo kila mmoja anaingiza miguu yake, tena wengi haina soksi, Maana yake ni nini? Kama mmojwapo ana athari, basi inawaangukia wengi.

Kwa kufanya hivyo, ni hali inayoweza kuwasababishia madhara ya maradhi ya kuambukizana, kupitia mabuti hayo.

Ni aina ya simulizi ya madhara yanayoweza kumfika mtu, kutokana na kuosha watu miguu sokoni. Ni maji yanayoachwa katika kitendawili. Hilo hatuna uhakika, kama ni majisafi na salama kweli.

Kikubwa kinachotakiwa sasa ni kwa wachuuzi hao wa sokoni Mabibo, wafanye shughuli zao kwa kuzingatia afya za walaji, uboreshaji wa maeneo yao hayo, ambako ndio hasa mzizi wa riziki zao.

# TANGAZO

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
*benki kwa maendeleo yako*

### AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa sasa 2020 | Mwaka uliopita 2019 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 11,959 | 10,317 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 13,900 | 15,679 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 22,770 | 25,039 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 17,178 | 211 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 40 | 22 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 26 | (4) |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 0 | 0 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 77,703 | 84,745 |
| 12 | Mali Nyingine | 11,310 | 10,997 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 39 | 20 |
| 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 14,813 | 22,376 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **169,739** | **169,401** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 1,511 | 3,361 |
| 18 | Amana za Wateja | 118,304 | 107,111 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana Maalumu | 0 | 0 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 1 | 2 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 3,075 | 2,820 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa | 8,192 | 7,307 |
| 27 | Dhima Nyingine | 9,478 | 15,322 |
| 28 | Madeni | 713 | 12,086 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **141,274** | **148,010** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29)* | **28,465** | **21,391** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 10,984 | 10,984 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (5,627) | 4,688 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 0 | 0 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 23,108 | 5,719 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **28,465** | **21,391** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 102 | 372 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 11,924 | 16,706 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 6,927 | 9,204 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 73 | 1,461 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 16.8% | 12.6% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 15.5% | 17.8% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 69.4% | 83.9% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 45.9% | 55.5% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 59.2% | 64.9% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 8.5% | -7.0% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 0.2% | 9.1% |

### AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI
### KWA MWAKA INAYOISHIA 31.12.2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Limbikizo la Mwaka wa sasa 2020 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 2019 |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 24,890 | 29,265 |
| 2 | Gharama za Riba | (7,804) | (6,803) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **17,087** | **22,461** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 0 | 0 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (4,405) | (1,824) |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **4,174** | **6,211** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 286 | 349 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 3,227 | 5,039 |
| | 6.3 Gawio | 0 | 0 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 661 | 823 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(25,156)** | **(28,074)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (13,057) | (14,645) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 0 | 0 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (12,099) | (13,428) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(8,301)** | **(1,226)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (1,617) | (1,663) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(9,918)** | **(2,889)** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | 0 | 0 |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(9,918)** | **(2,889)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 418 | 429 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (903) | (263) |
| 15 | **Idadi ya Matawi** | **18** | **18** |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -2.5% | -1.8% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -16.7% | -13.3% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 120.4% | 96.7% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 15.0% | 20.4% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA
### KWA MWAKA ULIOISHIA 31.12.2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Limbikizo la Mwaka wa sasa 2020 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 2019 |
|---|---|---|---|
| **I:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (8,301) | (1,226) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | |
| | - Hasara Katika Mali | 7,630 | 5,604 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 2,086 | (3,922) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | 0 | (3) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 9,874 | (7,921) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 2,680 | 1,531 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 351 | (599) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (10,855) | 3,865 |
| | - Kodi Iliyolipwa | (1,877) | 0 |
| | - Mengineyo (bainisha) | 1,704 | 2,208 |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | **3,292** | **(463)** |
| **II:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| | Gawio Lililopokewa | 0 | 0 |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (133) | (427) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | (19) | 3 |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 |
| | Mengineyo (bainisha) | 0 | 0 |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | **(152)** | **(424)** |
| **III:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 16,992 | 2,377 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 0 | 0 |
| | Mengineyo (bainisha) | (2,497) | (2,450) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **14,495** | **(73)** |
| **IV:** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 17,635 | (960) |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 18,624 | 19,584 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **36,259** | **18,624** |

### AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31.12.2020

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2020** | **10,984,416** | **2,431,917** | **4,687,639** | **3,286,944** | **-** | **0** | **21,390,916** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapa | 0 | 0 | (9,917,878) | 0 | 0 | 0 | **(9,917,878)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | (396,750) | 396,750 | 0 | 0 | **0** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mengineyo (Tangulizi la mtaji wa Hisa) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 16,992,072 | **16,992,072** |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2020** | **10,984,416** | **2,431,917** | **(5,626,989)** | **3,683,694** | **-** | **16,992,072** | **28,465,109** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2019** | **8,607,135** | **2,431,917** | **7,546,745** | **2,537,257** | **779,217** | **0** | **21,902,271** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapa | 0 | 0 | (2,888,636) | 0 | 0 | 0 | (2,888,636) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Miamala na wanahisa | 2,377,281 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2,377,281 |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | (749,687) | 749,687 | 0 | 0 | 0 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 779,217 | 0 | (779,217) | 0 | 0 |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2019** | **10,984,416** | **2,431,917** | **4,687,639** | **3,286,944** | **0** | **0** | **21,390,916** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA MWAKA UNAYOISHIA 31.12.2020

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| *Jina* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| **1.** | **Ernest Massawe** | |
| **2.** | **Dr. Josephat Lotto** | |

**Sasa unaweza kulipia malipo yote ya Serikali (GePG) na Kodi za TRA kupitia Akiba Mobile na Matawi yetu yote ambayo hayana foleni."**

MAHOJIANO MAALUM

# Dk. Hosea: Kwanini ninafaa kuwa Rais TLS

**Na Mwandishi wetu**

ALIYEKUWA Mkurugenzi wa Taasisi ya Kupambana na Rushwa Tanzania, Dk. Edward Hosea (pichani), ameeleza ni kwanini anaona anatosha katika nafasi ya rais wa chama cha wanasheria Tanzania (TLS) kurithi mikoba ya Rugemeleza Nshala.

Aidha, ameeleza atakachoteta na Rais Samia Hassan Suluhu, ikiwa atapata nafasi ya kuzugumza naye ana kwa ana kwa nafasi yake ya rais wa TLS.

Katika mahojiano na Nipashe, Dk. Hosea anaeleza mikakati yake ya kuifanya TLS kuwafikia Watanzania kwa kutumia teknolojia ya kisasa, ili kutatua kero mbalimbali zinazohitaji msaada wa kisheria.

**Swali:** Kipi kimekusukuma kugombea nafasi ya urais TLS?

**Jibu:** Kwanza ni haki yangu kidemokrasia ndani ya TLS kuwa mtu yeyote anaweza kugombea.

"Pili, ninawiwa, nawiwa kwelikweli kwamba chama hiki kinahitaji mtu mzoefu na amepitia serikalini, anajua serikali inavyofanya kazi zake."

"Nimefanya kazi mahakama, nilikuwa hakimu mkazi na nafasi ya mwisho nilikuwa Kaimu Msajili nilipokuwa mahakamani Mtwara, lakini pia, nimeshiriki shughuli nyingi katika Bunge nimeitwa kuhojiwa katika mabunge kama Mkurugenzi wa TAKUKURU."

Nina uzoefu wa kujua Bunge linafanyaje kazi, na ili upitishe mswada au upeleke hoja, protokali za serikali nazijua na kwamba kuna vitu lazima ujue jinsi ya kuongea na serikali. Sioni vibaya kukisaidia chama hiki.

Pia nimefanya kazi na mahakama, nimetenda haki, mtu alipotakiwa kufungwa nimefunga na alipotakiwa kuachiwa aliachiwa, kwahiyo siyo kwamba naongea tu, ni vitu nilivyoviishi.

Chama chetu kinahitaji mtu wa aina yangu, na niseme kazi ya urais TLS siyo ya mshahara kama watu wanavyofikiria, mimi nimestaafu, lakini sijachoka, na bado nina nguvu ya kusaidia kitaaluma.

Nimewahi kufanya kazi huko nyuma na naamini nitaisaidia TLS kufanya vitu ambavyo havihitaji nguvu nyingi. Mambo mengi ni ya kiutawala tu, najua utawala ni nini, najua sera ni nini na najua sheria ni nini. Nadhani ni muda mwafaka wa kuwa na mtu kama mimi, nadhani Mungu ananipa wito ili niwatumikie.

Mimi Mungu amenibariki sana, amenipa wito kama wenzangu watahitaji niwatumikie, mbali na kuwa Mkurugenzi wa TAKUKURU nimefanya kazi na vyombo vya kimataifa, nimekuwa rais wa kwanza wa vyombo vya kupambana na rushwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), nilichaguliwa kuwa rais wa vyombo vya kupambana na rushwa katika nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), na pia nilichaguliwa kuwa rais wa vyombo vya kupambana na rushwa katika Jumuiya ya Madola Afrika, kana kwamba haitoshi nilikuwa rais wa bodi ya kupambana na rushwa katika Umoja wa Afrika (AU), mpaka nastaafu nilikuwa makamu wa rais wa vyombo vya kupambana na rushwa duniani, sasa wale wanaojaji sasa nilifikaje hapa kama ningekuwa mbabaishaji tu, yaani dunia wananiona nafaa hapa nyumbani nionekane sifai, Mungu alinipendelea na nilitumia weledi wangu kuisaidia Tanzania, na kwa wakati wangu Tanzania ilikuwa inaonekana katika mapambano dhidi ya rushwa.

**Swali:** Baadhi ya wagombea wenzako na washabiki wa wagombea, wanakupinga kwa hoja kwamba umekuwa mtu wa mfumo, mahakamani, TAKUKURU na kipindi fulani TLS kimekuwa ni cha kiharakati cha kupambana na mfumo uliokuwapo. Unadhani kinahitaji kuendeshwa kwenye mapambano zaidi au majadiliano zaidi.

**Jibu:** TLS kinatawaliwa na malengo ya kifungu cha 4 cha sheria inayoanzisha TLS au sura ya 307 ya sheria za Tanzania, na yale ndio malengo yanayompambanua mtu yeyote anayetaka kuiongoza.

Ukisoma kifunga cha nne A mpaka E, ndo hayo mambo ya utawala wa sheria, kuheshimu sheria na kila mtu yuko sawa katika macho ya sheria kutetea raia, kutetea wanasheria wenzetu wanapokumbwa na matatizo mbalimbali, kuishauri serikali, kushirikiana na mahakama, yote yametajwa pale.

Elimu endelevu kwa ajili ya wanasheria yametajwa kisheria wala sio mawazo ya mtu, lakini ukimalizia katika vifungu vinavyobaki ni suala la uwekezaji. Kwamba TLS iangalie ni namna gani ya kuwekeza ili iweze kujiendesha, na kwamba ni moja ya vitu alivyovipa kipaumbele ili iweze kujiendesha kiuchumi.

Na moja ya vitu ambavyo nimependekeza ambavyo kwangu mimi ni 'quick wins' (ushindi wa haraka), tuna jengo la Wakili House, inamaana ya kwamba tunaweza kukopesheka, kwa mawazo yangu, tunahitaji kuwa na kiwanja kikubwa Dodoma, makao makuu ya nchi ili tujenge ukumbi mkubwa wa kisasa wa mikutano, lakini pembeni kuwe na 'Lodge' ili watu wakija kwenye mkutano wawe na mahali pakulala, kula na vitu kama hivyo, yawezekana kabisa.

Tunayo 'title' (hati) na benki haiwezi kushindwa kuikopoesha TLS tukawekeza, kwahiyo ndani ya mwaka wangu mmoja nataka tuwekeze, ili kupunguza gharama za wanachama wetu ambao wanatumia gharama nyingi kuiendesha TLS, hiyo ni moja.

Kuhakikisha TLS inaanzisha utaratibu wa kuwasiliana na wateja wake (wananchi na yeyote) mwenye



kutaka huduma zetu kwa mfumo wa E-Legal (mfumo wa kidigitali), mfano mtu yupo Kigoma na anahitaji mambo ya usia, anasumbuliwa na ndugu na jamaa, huyu ni mama ameachwa na mumewe, lakini anapewa shida tu, sasa wakili anampataje?

Kama ana vijana wamesoma anaingia kwenye mtandao, tuna wanasheria wamebobea ndani ya TLS, kwahiyo nataka kuanzisha huo utaratibu kwamba mwananchi hahitaji kwenda kumuona wakili ofisini, akiwa hapo hapo nyumbani. Itasaidia kupata mapato, kuwafikia watu wengi, kodi ya serikali inakusanywa kwa haraka."

TLS inahitaji pia kuweka mfumo mzuri wa mashauri yanayoamriwa na mahakama za juu za Tanzania, lakini tunahitaji pia kuwa na mfumo wa uamuzi mbalimbali ya jumuiya ya madola, kwahivyo haya mimi nayaita quick wins.

Moja ya mambo ambayo wanachama wetu wanayalalamikia ni suala zima la bima, upo utaratibu uliopo sasa hivi wa bima, ambao tumeshindwa kuukamilisha kwasababu anayetaka kutoa bima anataka mpaka tufikie idadi fulani ya watu, tupo kwenye dunia ya ushindani hatuhitaji hayo masharti.

"Nimeshalifanyia kazi ya kutosha na tayari yapo makampuni(kampuni) ya bima yapo tayari kuwapa wanachama wetu bima bila masharti, hayo ni machache tu ambayo nikiingia mimi mwaka mmoja nipo tayari kuyafanya hayo yatokee, kwasababu nina uzoefu, lakini nimeyafanyia kazi," alisema.

"Mimi nataka kutumikia huduma ya bure, siingii ndani ya TLS kuomba mshahara, na kazi ya rais TLS ni kama mwenyekiti wa bodi, kazi ya rais ni kuweka uongozi imara ambao unatambua mifumo, taratibu na sheria na vyote hivi mimi nimeishi.

Siwezi kubeza jitihada za watangulizi wangu kwa kuwa wamefanya kazi nzuri, na kwa sasa ndiye kiongozi ninayefaa, kama watanikataa ni kwa sababu zao, lakini siyo kwamba wamekosa kiongozi, huu ndio muda sahihi wa kupata kiongozi mwenye uzoefu, mimi sina cheo cha siasa, nilikuwa kiongozi wa umma.

**Swali**: Ukipata nafasi ya kukutana na Rais Samia, mambo gani utamshauri?

**Jibu:** Nitasubiri nikichaguliwa, sitaki kuongea vitu kabla ya kuchaguliwa, lakini ninayo ambayo nimeyaandaa na naamini kabisa Rais Samia kwa namna ambavyo namsikiliza mimi, naona kwamba ana utu na anaelewa shida za Watanzania, anaelewa yapo mambo tunapaswa tuyatazame upya.

Kama yeye anazungumza hivyo naamini bado kuna nafasi ya mashauriano. TLS sio yatima kwa Tanzania, ni sehemu ya Watanzania, bila TLS hizi sheria inakua shida, anayeenda mahakamani nani? Ni wanasheria.

**Swali:** Kuna baadhi ya watu wanasema wewe ni mkaidi sana, mbabe, ukiwa na jambo lako haurudi nyuma, hilo ndio lililokufanya uondoke TAKUKURU kwasababu hukukubali kuburuzwa, hata ulipokuwa msaidizi wa Jaji Nyalali ulitofautiana naye kwasababu ya kuona baadhi ya vitu haviendi sawa.

**Jibu:** Sijui kama ni mbabe, wananisingizia. Kifungu cha 37 cha kuzuia na kupambana na rushwa kinanizuia kuongea mambo ya undani ya serikali, naheshimu na nilikula kiapo, siwezi kuongea mambo ya ndani ya serikali.

Niseme tu, mimi siyo kwamba ni mbabe, nina kitu nakiita principles, tukikubaliana A, B, kesho ukasema C, D napata shida, sio leo umesema hivi na kesho umesema vile, uongozi ni kutoa dira na kuwaonyesha watu unapotaka kufika, haiwezekani leo umesema utaenda kushoto kesho ukasema twendeni kulia, hiyo mimi napata shida yawezekana ndio maana naitwa mbabe.

Naamini katika sheria zilizowekwa, ukiwa kiongozi soma sheria zinazotawala chombo unachokiongoza, kwahiyo kama sheria inaniambia hivyo namimi nitasimama kwenye hiyo sheria na kwa bahati nzuri mimi ni mwana sheria. Shida ya tafsiri ni kwamba wakati mwingine unaonekana wewe ni mkaidi, sio ukaidi ni sheria, sasa nikisema sheria inasema hivi naambiwa mbabe basi uamuzi ni wao.

**Swali:** Katika kipindi chote ulichokuwa TAKUKURU, na kuna wakurugenzi kama wanne wamepita baada ya wewe kuondoka, ukipata nafasi ya kushauri chombo hiki cha umma namna bora ya kufanya shughuli zake kwa uzoefu wako ungewashauri nini?

**Jibu:** Ningeanza kwenye taarifa ya Tume ya Jaji Warioba, nataka nishauri mtu yeyote anayetaka kuzungumzia mambo ya rushwa hiyo ndiyo 'bench mark' ya Tanzania, nadhani tunaisahau tu hii taarifa. Ukiisoma ile taarifa ndio iliyopelekea kuzaa PCCB (Preventing and Combating of Corruption Bereau) kutoka PCB (Prevention of Corruption Bureau), tulichokifanya baada ya Tume ya Warioba tulikuwa tunaenda hatua kwa hatua kutekeleza mapendekezo ya tume hiyo.

Moja ni Capacity building ya PCCB, utakuaje na askari haujampa silaha unategemea ashinde vita? Lazima uajiri watu, lazima uwe na mafunzo, tulifanya hiyo. Ni kitu kimoja kuwa na jeshi, lakini ni kitu kingine kuwa na askari wenye mafunzo.

Zamani huduma ya TAKUKURU ilikuwa inaishia kwenye kanda, lakini tukaipeleka mpaka mikoani na wilayani.

Pili, uwezo wa kisheria, tulikuwa na mawakili zaidi ya 120 kwasababu unaopoenda mahakamani fahamu sheria na silaha ya pili ushahidi. Nashauri wenzangu kwamba usipeleke kitu hakijawiva, bora uonekane umechelewesha kuliko kupeleka mahakamani kitu hakijawiva, usipeleke kitu mahakamani ukasema bado tunaendelea na uchunguzi, ndio maana ya utawala wa sheria, mtu yeyote kama unamtuhumu bila mahakama kutoa uamuzi hauwezi kusema ni mwizi, mwenye kutoa uamuzi ni mahakama.

Ushauri wangu kesi zote ambazo zinaonekana zina ushahidi, zinaenda kwa DPP anazichuja na kutoa uamuzi, akishaona kuna ushahidi kesi inaenda mahakamani, ndio utaratibu.

**Swali:** Umekuwa TAKUKURU tangu 1995 hadi 2016, sasa umetoka kutumia elimu yako kuwa wakili wa kujitegemea, umejifunza nini ndani ya TLS kuhusiana na uwakili?

**Jibu:** Katika ilani yangu nimeweka angalizo, nimesema utu ni muhimu, sisi wanasheria tukiifuata hii dhana basi tutakuwa tumelifanyia taifa letu jambo kubwa sana kwa jamii, kama wewe ni wakili, yeyote anayekuja tanguliza utu, tunapokwenda mahakamani kwenye kesi tutumie dhana ya utu, ni haki mtuhumiwa akae rumande miaka mitano anasubiri kesi kuanza kusikilizwa? Mwalimu Nyerere alisema kuhusu utu, Kwame Nkurumah alisema, Nelson Mandela alisema, na wenye falsefa ya ubuntu wamesema, jamii imuone binadamu kwa utu wake hata kama anatuhumiwa.

Bunge litunge sheria zinazomuangalia mtu kwa utu wake, mahakama inapotoa uamuzi, itoe kwa kumuangalia mtu na utu wake, na sisi kama TLS tujaribu kuwa watu. Uwajibikaji na uwazi zaidi kwenye jamii pamoja na uadilifu.

# Kilombero yachakata mamilioni tani za miwa

**Na Gwamaka Alipipi**

KAMPUNI ya Sukari Kilombero kwa mara ya kwanza imefanikiwa kuchakata tani 1,409,995 za miwa kwa msimu wa mwaka 2020/2021, huku asilimia 48 ya miwa hiyo ikiwa ni ya wakulima wa bonde la Kilombero.

Idadi hiyo inazidi ya msimu uliopita za uchakataji wa miwa kwa zaidi ya tani 290,000.

Mkuu wa kitengo cha Mawasiliano Kampuni ya Sukari Kilombero, Joseph Rugaimukamu, alieleza mafanikio hayo na kufafanua kuwa uchakataji wa kiwango hicho ni mara ya kwanza kwa kiwanda hicho.

Alisema msimu wa uzalishaji wa mwaka 2019/2020, kiwanda kilichakata tani 1,120,059 za miwa.

Rugaimukamu alisema uzalishaji wa msimu uliopita uliathiriwa na mvua kubwa zilizoanza kunyesha oktoba, 2019 na kusababisha mafuriko kwenye mashamba ya miwa, daraja dogo la kiwanda na kuharibika kwa miundombinu iliyoathiri usafirishaji wa miwa kwenda kiwandani.

Alibainisha kwamba msimu wa mwaka 2020/2021 uliofikia ukingoni hivi karibuni, Kampuni ya Sukari Kilombero, imezalisha tani 123,167.5398 za sukari, takwimu ambayo ikaribiana na lengo la uzalishaji sukari msimu huo ambao ni tani 127,871 za sukari.

"Hii ni mara ya kwanza viwanda vyetu vimefanikisha kuchakata miwa kwa kiasi kikubwa kama hichi, mara ya mwisho tuliyokaribia kufikia rekodi hii ni mwaka 2014 ambapo tulifanikiwa kuchakata tani 1,356,549 za miwa," alisema Rugaimukamu.

Alieza kuwa pamoja na kuchakata miwa mingi zaidi, kiwango cha sukari iliyozalishwa hakikuwiana na kiwango cha miwa iliyochakatwa kutokana na ubora wa miwa ambayo ilikuwa na kiwango kidogo cha sukari, pamoja na kukaa bila kuchakatwa tangu msimu wa mwaka 2019/2020.

"Ingawa hatukufikia lengo letu la uzalishaji wa sukari, tumefarijika kufanikisha kuchakata miwa mingi zaidi ya wakulima, hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa kiwango cha miwa kitakachobaki msimu ujao," alisema Rugaimukamu na kuongeza:

"Hii inatuweka kwenye nafasi nzuri ya kuanza msimu ujao na miwa yenye viwango vizuri, kwa hiyo tunatumaini tutaweza kupata sukari nyingi".

Alisema kwa msimu ujao, unaotarajiwa kuanza Mei mwaka huu, Kampuni ya Sukari Kilombero inatarajia kuzalisha tani 125,096 za sukari.

Aidha, alisema menejimenti ya Kampuni ya Sukari Kilombero iko kwenye mchakato wa kupata kibali kutoka kwa wanahisa ili kuweza kufanikisha mradi wa upanuzi wa kiwanda.

Alisema upanuzi huo unatarajiwa kuongeza kiwango cha uchakataji wa miwa na uzalishaji wa sukari zaidi ya mara mbili, na hatimaye kupunguza uhaba wa sukari nchini.

# TAKUKURU yaingilia kati sakata DED kutishiwa maisha

**Na Thobias Mwanakatwe, SONGWE**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Songwe (TAKUKURU), imesema itaanza uchunguzi kuhusu sakata la malipo ya Sh. milioni 12 zinazodaiwa kutaka alipwe kiongozi mmoja wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani humo.

Kamanda wa TAKUKURU Mkoa wa Songwe, Damas Suta, akizungumza na gazeti hili jana, baada ya kupata taarifa za tukio la Mkurugenzi kutishiwa maisha kutokana na kukataa kuidhinisha malipo ya Sh. milioni 12 anazotaka kulipwa kigogo wa CCM, taasisi hiyo itaanza kuchunguza suala hilo haraka.

"Mimi nipo safari, ngoja nimwagize Naibu Kamanda alitafute gazeti ili tuanzie hapo maana sisi taarifa zetu tunazipata kwa njia mbalimbali yakiwamo magazeti, tutamwita Mkurugenzi aeleze sababu za kutishiwa kwake na baadaye kulichunguza kwa kina," alisema.

Suta alisema iwapo Mkurugenzi huyo wa Halmashauri atajichanganya na kulipa fedha hizo kwa kigogo wa CCM kwasababu ya kutishiwa maisha atatakiwa kuhojiwa na TAKUKURU.

"Kama... (anamtaja jina) alisupply vifaa kwenye jengo la mtu binafsi halafu aende kudai fedha kwa mkurugenzi hiyo siyo sahihi, na sisi tutaingia tu pale Mkurugenzi atakapolipa fedha hizo," alisema.

Alisema kama mkurugenzi atalipa fedha hizo kwa kigogo huyo wa CCM, TAKUKURU itahitaji ripoti ya uchunguzi ya kamati ya ujenzi ili kujiridhisha kama vifaa hivyo vilikuwa sahihi na pia wataulizwa mashahidi waliokuwapo katika jengo hilo.

Kutokana na sakata hilo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, Hanji Godigodi alitoa taarifa katika kituo kikuu cha polisi Vwawa na kupewa namba MBZ/IR/200/2021 baada ya kudai kutishiwa maisha na kigogo huyo wa CCM.

Mkurugenzi huyo alidai kutishiwa maisha mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe na Katibu Tawala wa Mkoa huo, baada ya kumalizika kwa kikao cha Bodi ya Barabara ya Mkoa.

Godigodi alisema amekataa kuidhinisha malipo hayo kwa kigogo huyo wa CCM kwasababu ameshindwa kuwasilisha nyaraka zinazoonyesha kama kweli alisambaza vifaa ambazo ni nondo na saruji katika halmashauri hiyo.




Mkurugenzi wa Biashara wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), Elvis Ndunguru (katikati waliokaa) pamoja na Mkurugenzi wa Fedha wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), Derick Lugemala wakitia saini mkataba wa makubaliano wa kufanya kazi pamoja kwaajili ya kuwawezesha wakulima wadogo katika minyororo ya thamani ya kilimo, jijini Dar es Salaam juzi. Wanaoshuhudia ni Meneja wa Mfuko Maalum wa Dhamana kwa wakulima wadodo kutoka TADB, Asha Tarimo (kulia) na Mkurugenzi wa sheria wa TADB, Dk. Edson Rechungura. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kasi ndogo wakimbizi kurejea Burundi yashtua

**Na Deogratius Nsokolo,** KIGOMA

KASI ndogo ya kurejea Burundi kwa wakimbizi wa nchi hiyo waliopo mkoani Kigoma kumeishtua serikali, hivyo imetaka zoezi hilo liende haraka kwa sababu hivi sasa nchi hiyo ina amani na inawahitaji raia wake.

Mkuu wa Mkoa wa Kigoma , Thobias Andengenye, akizungumza baada ya kutembelea kambi ya wakimbizi wa Burundi Nyarugusu wilayani Kasulu, alisema haridhishwi na idadi ndogo ya wakimbizi wanaorejea, na kuagiza Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia Wakimbizi (UNHCR) kuhakikisha zoezi hilo linafanyika kwa uwazi.

Akiwahutubia wakimbizi wa Burundi kambini hapo, alisema suala la ukimbizi lina mwisho, hivyo ni muhimu wakatambua hali hiyo kutokana na uamuzi wa pande zote zinazohusika na suala la wakimbizi ambazo ni UNHCR , Serikali ya Burundi na Serikali ya Tanzania.

"Tunahitaji muende kwenu mkajenge nchi yenu, taifa lenu linawahitaji sana, ni vizuri mkatambua hivyo na kufanya uamuzi wa kuondoka kwa hiari, badala ya kuendelea kukaa wakati nchi yenu ina amani ya kutosha, hii haikubaliki," alisema na kuongeza:

"Wakati ni sasa chukueni hatua, Burundi ni shwari mnatakiwa mrudi kwa hiari, Watanzania wanawapenda sana, lakini ni lazima mrudi ili msaidie kuijenga nchi yenu."

Mapema Kaimu Mkuu wa Kambi ya Wakimbizi Nyarugusu, Miraji Chagonja, alisema kambi hiyo yenye wakimbizi 53,856 toka Burundi, katika kipindi cha kuanzia Septemba mwaka 2017 hadi Machi 2021 ni wakimbizi 20,586 kutoka kambi hiyo ndio wamerejea kwa hiari kwao.

Alisema idara ya huduma kwa wakimbizi kwa kushirikiana na UNHCR wamekuwa wakiendesha kampeni mara kwa mara za kuwahamasisha wakimbizi kurejea Burundi, lakini bado kasi yao ni ndogo, hali inayotia shaka kama watamalizika.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Huduma kwa Wakimbizi toka Wizara ya Mambo ya Ndani, Sudi Mwakibasi, alisema viongozi wa Tanzania na Burundi wamekutana mara kadhaa na kuazimia wakimbizi warejee kwa hiari.

Alisema uchunguzi wa awali wa idara hiyo umebaini wakimbizi wa Burundi walio wengi hawana sababu za msingi zinazowafanya waendelee kuwapo nchini, kwa kuwa nchi yao ina amani na usalama, na kwamba sababu inayoonekana ni hali ya uchumi.

"Kwa kweli hawana sababu ukilinganisha na wenzao wa DRC ambao wao bado hali si njema kwao," alisema Mwakibasi.

Mkuu wa UNHCR Kasulu, Ben Diallo, wamekuwa na jitihada za kuhamasisha wakimbizi kurejea na kila Alhamisi wanasafirishwa kwenda Burundi.

Alisema kinachokwamisha ni utayari wa Burundi kupokea idadi kubwa ya wakimbizi na kutimiza mahitaji yao kwa mujibu wa utaratibu.

Mmoja wa wakimbizi waliokuwa tayari kuondoka kwa hiyari, Nyandu Claude, alisema yeye na familia yake wameamua kuondoka kwa hiari ili kwenda kuishi Burundi na kusaidia ujenzi wa nchi yao, ambayo inatakiwa kujengwa na wananchi wote.

Kambi ya wakimbizi wa Burundi ya Nyarugusu inahifadhi pia wakimbizi 78,716 toka DRC, hivyo kuwa na idadi ya jumla ya wakimbizi 132,711.

TANGAZO

BancABC part of atlasmara

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

## IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### TAARIFA YA UKAGUZI WA WARAKA MIZANIA KWA MWAKA 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mwaka wa sasa 31-Dec-20 | Mwaka uliopita 31-Dec-19 |
|---|---|---|
| **A MALI** | | |
| 1 Fedha Taslimu | 3 289 | 3 572 |
| 2 Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 7 028 | 12 790 |
| 3 Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 43 178 | 33 052 |
| 4 Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 111 923 | 97 838 |
| 5 Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 Mikopo Halisi Iliyopo | 133 952 | 127 755 |
| | - | - |
| 12 Mali Nyingine | 27 803 | 26 548 |
| 13 Uwekezaji wa Hisa | 1 000 | 1 000 |
| 14 Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 6 583 | 6 639 |
| **16 JUMLA YA MALI** | **334 756** | **309 194** |
| **B DHIMA** | | |
| 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 106 624 | 92 642 |
| 18 Amana za Wateja | 111 082 | 99 021 |
| 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 Amana Maalumu | - | - |
| 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 Dhima Nyingine | 2 961 | 4 356 |
| 28 Madeni | 74 640 | 69 553 |
| **29 JUMLA YA DHIMA** | **295 307** | **265 571** |
| **30 MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **39 449** | **43 623** |
| **C FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 105 114 | 105 114 |
| 32 Hisa za Upendeleo | 17 840 | 17 840 |
| 33 Akiba ya Mtaji | - | - |
| 34 Hifadhi ya hatari ya benki kuu | 2 274 | 130 |
| 35 Mapato Yaliyobakizwa | (86 821) | (80 526) |
| 36 Akaunti Nyingine za Mtaji | 989 | 1 065 |
| **37 JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **39 396** | **43 623** |
| 38 Dhima Zisizo Dhahiri | 2 866 | 3 137 |
| 39 Mikopo Chechefu | 19 585 | 17 957 |
| 40 Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 15 128 | 15 351 |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 11.77% | 14.11% |
| (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 13.14% | 12.55% |
| (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 68.48% | 74.67% |
| (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 44.53% | 41.32% |
| (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 48.30% | 83.65% |
| (vi) Ongezeko la Amana | 12.18% | -4.18% |
| (vii) Ongezeko la Mali | 8.27% | -3.56% |

### TAARIFA YA UKAGUZI YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mwaka wa sasa 31-Dec-20 | Mwaka uliopita 31-Dec-19 |
|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 42 736 | 40 926 |
| 2 Gharama za Riba | (19 652) | (19 013) |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **23 084** | **21 912** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (1 278) | (4 052) |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **5 991** | **7 907** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 1 326 | 1 901 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 4 665 | 6 006 |
| 6.3 Gawio | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | - | - |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **(31 803)** | **(34 392)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (10 473) | (10 842) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | (1 077) | (1 829) |
| 7.3 Gharama Nyingine | (20 253) | (21 721) |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(4 006)** | **(8 624)** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | (145) | (145) |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(4 152)** | **(8 769)** |
| 11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | 76 | - |
| **12 Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(4 076)** | **(8 769)** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 144 | 154 |
| 14 Mapato kwa Hisa | -39% | -83% |
| 15 | 0% | 0% |
| 16 Idadi ya Matawi | 6 | 7 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (I) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -1.20% | -2.74% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -10.17% | -18.30% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | -109.38% | -115.33% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 2.11% | 8.47% |

### TAARIFA YA UKAGUZI YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA DESEMBA 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mwaka wa sasa 31-Dec-20 | Mwaka uliopita 31-Dec-19 |
|---|---|---|
| **I Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | (4 006) | (8 624) |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - |
| - Hasara Katika Mali | 5 380 | 7 151 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (8 017) | 14 403 |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 26 044 | (8 357) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (10 127) | 7 558 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (1 395) | (947) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (746) | (5 206) |
| - Kodi Iliyolipwa | (135) | (198) |
| - Mengineyo (bainisha) | - | 927 |
| **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **6 998** | **6 707** |
| **II Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (4 046) | (3 540) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(4 046)** | **(3 540)** |
| **III Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | 6 940.00 |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 5 087.55 | 4 878.08 |
| Mengineyo (bainisha) | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **5 088** | **11 818** |
| **IV Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 8 040 | 14 986 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 87 766 | 72 780 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **95 806** | **87 766** |

### TAARIFA YA UKAGUZI YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2020

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **122 954** | **-** | **(80 525)** | **130** | **0** | **1 065** | **43 623** |
| Marekebisho yatokanayo na IFRS 9 | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la kodi litokanalo na IFRS 9 | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwanzo wa mwaka lilorekebishwa** | **122 954** | **-** | **(80 525)** | **130** | **0** | **1 065** | **43 623** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (4 152) | - | - | - | **(4 152)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | (2 144) | 2 144 | - | (76) | (76) |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **122 954** | **-** | **(86 820)** | **2 274** | **0** | **989** | **39 396** |
| | | | | | | | - |
| **Mwaka Uliopita 2019** | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **116 014** | **-** | **(67 756)** | **-** | **1 284** | **1 065** | **50 607** |
| Marekebisho yatokanayo na IFRS 9 | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la kodi litokanalo na IFRS 9 | - | - | (5 154) | - | - | - | **(5 154)** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (8 769) | - | - | - | **(8 769)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 6 940 | - | - | - | - | - | **6 940** |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (130) | 130 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 1 284 | - | (1 284) | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **122 954** | **-** | **(80 525)** | **130** | **0** | **1 065** | **43 623** |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi. Taarifa hizi za fedha zimekaguliwa na Ernst & Young , Certified Public Accountants (T) kupokea taarifa huru ya uhakiki wa ukaguzi.

Taarifa hizi za fedha ziliidhinishwa na bodi ya wakurugenzi siku ya tarehe 26 Machi 2021


**I. John**

**(Mkurugenzi mtendaji)** **Imesainiwa tarehe 14 April 2021**

**Mr. R. Dave**

**(Mkurugenzi)**

ama
ALHAMISI APRILI 15 2021
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12
**Tumeboresha hivi nyendo za maji kwa mchoro wa 1980**

MTETEZI CONSOLATHA:

# Fahamu orodha ya ukatili wapatao kinamama walioko kazini sokoni

**Na Yasmine Protace**

UKATILI ni neno moja, lakini kina mapana zaidi hasa inapochambuliwa aina za ukatili ambazo zipo na zinafanywa na watu waliotuzunguka.

Kumekuwapo na ukatili wa kupigwa na wengine wanakeketwa, kubakwa au kulawitiwa na aina nyingi na umekuwa ukifanywa maeneo mbalimbali yanayozunguka.

Ndani ya somo hilo, kunatajwa kuwapo ukatili mkubwa unaofanywa na wafanyabiashara wa chakula katika masoko.

Mkurugenzi wa Shirika la Wasaidizi wa Kisheria Sokoni ( Communite Alliance For Legal and Social Justis) Consolatha Cleophas, anakiri kuwapo aina tano zilizoko sokoni

Hapo katika orodha, kuna aina za ukatili wa kingono, wa kisaikolojia, kiuchumi, kimwili na kingono na katika masoko, wanawake wanaishi pasipo ridhaa .

"Huu ukatili unaofanywa sana sokoni, kwa mama lishe na anayekataa kushikwashikwa na wanaume wamekuwa hawanunui chakula chake," anasema Consolatha .

Anaongeza kwamba, ukatili huo pia kuna wanaoitwa 'dungadunga' na wamekuwa wakiwafanyia vitu vibaya, wanaokuja sokoni kuchagua nguo, pia kuna ukatili mwingine wanawake kushikwa ovyo na wauza mitumba.

Pia, katika soko la Ilala kuna ukatili ambao baadhi ya mafundi wa nguo wanawake, alipewa nguo za mitumba na wamejikuta wakitembea na wanaume, ili wawaletee nguo za kushona.

Anasema, ukatili wa kiuchumi unafanywa na baadhi ya watu kula chakula kwa mama lishe bila kulipa, ilhali wapishi wanachukua mahitaji yao dukani wakijua baada ya kuuza atarudisha pesa dukani.

Mama huyo anasimulia mkasa, namna wasichana wahudumu wa kupeleka chakula kwa wateja, hawalipwi hali inayofanya waajiri nao wasite kuwalipa posho zao.



Mkurugenzi wa Shirika la Wasaidizi wa Kisheria Sokoni, Consolatha Cleophas **PROTUS YASMINE**

Huko kwa wateja wakizidi kudai, hukutana na sharti la kuingia uhusiano wa kimapenzi, ikiwa ni sharti la malipo ya deni la chakula.

Mwajuma Ally, ni msambaza chakula katika Soko la Makumbusho, anasema wanakutana na adha ya kuwapa chakula madereva wa bodaboda, ambao hula chakula na kukimbia pale wanapoona wanaenda kudaiwa.

"Kitendo Cha kukimbiwa na bodaboda kinasababisha hama mimi malipo yangu sipati," anasema, hali inayowaangusha katika shida ya ngono kujikidhi kimaisha.

> **"Madalali wanawapa watu vitu na wamekuwa wakiwaingiza katika madeni. Kitendo hicho kinachangia kuwarundisha watu nyuma kiuchumi," anasema na kuongeza kuwa, pia kuna ukatili wa kisaikolojia mwanamama kutukanwa kila mara.**

### MADALALI SOKONI

Akizungumzia kuhusu madalali, Consolatha anasema pindi wanaposhusha mizigo na kupeleka kwa wachuuzi kupitia madalali, nako wanakutana na majanga hayo ya dai la rushwa ya ngono.

"Madalali wanawapa watu vitu na wamekuwa wakiwaingiza katika madeni. Kitendo hicho kinachangia kuwarundisha watu nyuma kiuchumi," anasema na kuongeza kuwa, pia kuna ukatili wa kisaikolojia mwanamama kutukanwa kila mara.

Anasema kutokana na matukio hayo ya kikatili, zimekuwa zikipelekwa kwa wenyeviti wa vitengo na zipo ambazo zinaisha kutokana na kusikilizwa kwa faini hadi Sh. 50,000.

Anasema, ukatili wa mwili, mtu anapopigwa ushauri wa kwenda polisi, ili mtuhumiwa achukuliwe hatua na wale' 'dungadunga' faini wanatozwa faini ya Sh. 50,000.

Kwa mujibu wa Consolatha, katika kipindi cha mwaka 2018 mpaka sasa, kuna jumla ya kesi 700 wameishapokea kutoka masoko yote ya Ilala na Temeke, jijini Dar es Salaam, ambako kuna wasaidizi wa kisheria.

Anasema, hadi sasa wanaendelea kutoa elimu, ikiwamo ya sheria za mikataba waliokwishawapatia baadhi ya wafanyabiashara, kutoka vitengo mbalimbali vya soko la Buguruni, ambako wameshachukua mikataba na kufanyia kazi.

### SOKONI ILALA?

Consolatha anasema, katika masoko likiwamo soko la Ilala, kuna kasoro hakuna kamati ya soko na inapotakiwa kufanyika mikutano, wafanyabiashara hadi sasa hawana sehemu ya kupelekwa shida zao, baada ya uongozi uliokuwapo kuvunjwa.

Anazungumzia Kitengo cha Karoti katika soko la Ilala wakati uongozi ulikuwapo, walikuwa wakiuza kiroba chenye uzito wa kilo 60 hadi 65 kwa mchuuzi mmoja, lakini sasa mauzo yameshuka hadi kati ya kilo 25 Hadi 30, huku madalali wanawadhulumu nao hawana chombo cha kuwasimamia. Mama huyo anahimiza elimu inahitajika katika maeneo ya soko

MAZINGIRA

MHANDISI MRADI BWAWA NYERERE:

# Tumeboresha hivi nyendo za maji kwa mchoro wa 1980, miamba hatukugusa

- Kubadilika miamba inahitaji miaka milioni 1
- Pia mawe, sasa zege; tuta Km. moja na robo



Shughuli za ujenzi wa chanzo cha umeme, Bwawa la Julius Nyerere, ikiendelea. **PICHA ZOTE: MTANDAO**.

**Na Beatrice Shayo**

"NI kweli kuna maneno yanayosemwa tumetumia upembuzi yakinifu wa mwaka 1970, kimsingi upembuzi yakinifu wa mwaka 1980 kwa sehemu kubwa ilihusishwa mwaka 2017 kwenye usanifu na michoro iliyotumika katika huu mradi wa umeme wa maji.

"Ni mpya na ndio zilitumika katika kutangaza tenda," anatamka Mshauri Mkazi wa Mradi wa JNHPP, Mhandisi John Mageni, akisema ni bwawa la kuzalisha umeme wa maji la Julius Nyerere lililopo Rufiji mkoani Pwani.

Awali ilijulikana kwa jina Stiegel's Gorge na matarajio ya uzalishaji ni megawati 2115 za nishati, hadi utakapokamilika, ukubwa unaochukua nafasi ya nne barani Afrika.

Mhandisi Mageni anasema, ujenzi unaoendelea unafanywa na makandarasi wawili, kampuni ya Arab Contractors za Misri na Elsewedy Electric, kutoka India, ikitarajiwa kugharimu Sh. Trilioni 6.5.

Pia, ni mradi unaotarajiwa kushusha bei ya umeme kutoka uniti moja inayouzwa kati ya Sh 400 hadi 600 kwa sasa na kuuzwa kwa Sh. 36.

**MCHORO WABADILIKA**

Mageni anaeleza wataalamu walifanya maboresho ya upembuzi yakinifu wa mwaka 1980 kuhusu miamba katika mradi huo, huku wakisimamia sayansi ya miamba inachukua takribani miaka 100,000 hadi milioni moja kwa tabia ya mwamba kubadilika.

Anafafanua: "Sasa tulikuwa na taarifa ya mwamba uliochunguzwa mwaka 1980 na sisi tumeanza kujenga miaka 37 baadaye.Tuliona taarifa zile zitaendana na uhalisia wa miamba iliyopo kwa sasa kwa sababu inachukua miaka elfu kwa mwamba kubadilika."

Mhandisi Mageni anafafanua kwamba, wamefanya maboresho makubwa katika usanifu na michoro na wamebadilisha aina ya bwawa lililopaswa kujengwa awali mwaka 1980, kwa kupanga mawe, sasa wakaendea kwenye bwawa la kupanga zege.

Pia, anasema wamebadili usanifu na michoro kwenye jengo la mitambo ya kuzalisha umeme upembuzi yakinifu ya mwaka 1980, iliyolenga kujenga vituo vitatu vya kuzalisha umeme (power house) kwa awamu ya miaka 20, ambayo mitambo ingezalisha megawati 2100.

"Tumejenga 'power house' jengo moja halipo chini ya ardhi, lipo juu ya ardhi na linabeba mashine tisa, wakati 'design' ( mchoro) uliopita ulikuwa unabeba mashine zaidi ya tisa na uwezo umezidi megawati 15.

"Tutajenga mitambo yenye kuzalisha megawati 2115. Unaweza kuona megawati 15 ni ndogo, lakini hizi megawati 15 ni umeme ambao unatumika kwa Mkoa wa Singida," anafafanua.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alipotembelea mradi wa umme, Bwawa la Nyerere.

**UCHEPUSHAJI MAJI**

Mhandisi Mageni anasema, wamebadilisha namna ya kuchepusha maji na mengi kuwa ya kisasa, akifafanua upembuzi yakinifu wa awali mwaka 1980 ulikuwa na njia tatu za kuchepusha maji; mbili kushoto na moja kulia.

Hata hivyo, anasema katika upembuzi yakinifu wa mwaka 1980 sayansi ya miamba haikubadiliki. Anasema: "Tulichokitumia pekee katika uchambuzi yakinifu ya mwaka 1980 ni historia au taarifa za uchunguzi za miamba, kwa sababu miamba huchukua miaka taribani 100,000 hadi milioni moja kubadilika.

"Sisi kwa taarifa iliyokuwepo ya miaka 37 tunavyoanza kujenga tumeona bado ni umri mdogo kuwepo mabadiliko ya tabia ya miamba,'" anasema

Anasema, mkandarasi katika uchunguzi wake alioufanya alivyoanza kujenga alizingatia taarifa ya miamba ya kisayansi na ndicho alichokikuta pasipo na mabadiliko na kazi kuendelea bila kusuasua.

**WATUMIA UMEME MAJI**

Mhandisi Mageni anasema uzalishaji umeme kwa kutumia maji ni chanzo nafuu kuliko vyote na rafiki wa mazingira.

Hadi sasa, barani Afrika kuna nchi zaidi ya mbili zenye aina hiyo ya mabwawa makubwa, ikiongozwa na Ethiopia, ambayo imeshirikishwa katika upembuzi yakinifu, mwaka 2017.

"Wale wana mabwawa mengi na wanatumia umeme wa maji kwa sehemu kubwa. Nchi nyingine ambayo inatumia sana umeme wa maji ni Angola na nchi za Afrika Magharibi Nigeria, Cameroon na Ghana. Pia, kwa nchi za Afrika Mashariki na Congo zina hiyo huduma," anasema.

**UTEKELEZAJI MRADI**

Mhandisi Mageni anasema, walianza kutembelea eneo lenye kingo nne ndogo zitakazotumika kuzuia maji yasitoke watakapoanza kujaza bwawa, akisifu ujenzi unaendelea ndani ya muda wa mpango kazi, utakaomilika mnamo Juni 16, mwakani.

"Tulitembelea eneo la daraja la kudumu litakuwa linavuka Mto Rufiji. Litakuwa ni daraja la pili katika madaraja yanayovuka Mto Rufiji," anasema, akitaja nyingine Daraja la Mkapa.

Anasema, robo ya jumla ya kazi imeshakamilika na nusu ya msingi umekamilika na matarajio daraja hilo litamalizika hadi kufika Januari mwaka ujao, ikiwa na uwezo wa kubeba vifaa vizito tani 100.

Mageni anasema kuna eneo linalojengwa la 'Power House; lenye urefu wa mita 400 upana mita 60 na kina cha kwenda juu ni mita 60 kazi inaendelea vizuri.

"Tutafunga mitambo tisa ya kuzalisha umeme na kila mtambo una uwezo wa kuzalisha megawati 235 jumla katika mitambo hiyo itazalisha megawati 2115 . Mitambo hiyo itazalisha umeme kwa kutumia maji njia ya kuleta umeme ipo katika hatua nzuri ya kukamilika,"

Anasema, katika mradi huo kuna tuta kuu lenye urefu wa kilomita moja na robo, itakayotekelezwa katika awamu kubwa mbili, yaani kunyanyua upande wa kushoto wa mto na kasha kulia kwake.

Anaitaja eneo la kupokea umeme au kuunganisha umeme wa gridi kutoka mfumo unaozalisha unaendelea vizuri, ikibakiza asilimia 10 kukamilisha.

"Tukimaliza 'foundation' (msingi) tunaanza kufunga vyuma ambavyo vitadhibiti, kupima na kuunganisha umeme kati ya Gridi ya Taifa na umeme wa mashine. Vifaa vyote vimeshaanza kutengenezwa na vingine vipo njiani vinakuja, inategemewa kufika kuanzia Julai mwaka huu," anasema.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, anasema makandarasi hao wa ujenzi wanazingatia viwango vya ubora na: "Kwa maeneo nyeti ya mradi yamekamilika kwa kiwango cha asilimia 47 na kipindi kilichobaki kinaweza kufika Juni mwaka 2022.

"Nimepata nafasi ya kutembelea eneo linalochemsha maji ambalo ni eneo la maporomoko ya maji kutakuwa na mitambo ya uzalishalishaji umeme, ambayo kazi nzuri nimeona iliendelea.

"Pia, nimeona daraja litakalotuunganisha pande mbili ujenzi wake unaendelea na wataalamu wetu wametuambia viwango vimezingatiwa,"

# Vyoo vinavyobaki nyenzo kuu ya kutetea afya

**Na Sabato Kasika**

VYOO vina mchango mkubwa katika kujenga afya bora, kwa kuwa ni huduma inayoweza kusababisha watu kujisaidia ovyo hata katika maeneo yasiyo rasmi na kusababisha maradhi, hata uchafuzi wa mazingira.

Ukosefu wa vyoo bora umekuwa ukitajwa kusababisha na magonjwa ya kuambukiza, ndiyo maana kumekuwapo na kampuni za kuhamasishha jamii kuwa na huduma hiyo nyumbani.

Wapo baadhi ya watu hasa maeneo ya vijijini, ambao huwa hawajengi vyoo na badala yake hujisaidia vichakani au kwenye mito na mabonde, hali ambayo inaweza kuhatarisha afya zao.

Katika kundi hilo, wapo ambao hataki tu kujenga vyoo na wengine ni kutokana na imani zao kwa kuwa wanaamini kwamba, ni makosa mtu kwenda kujisaidia katika choo, hivyo wanaona ni vyema waende vichakani.

Kuna baadhi ya vituko ambavyo mwendesha kampeni za 'Nyumba ni Choo' amewahi kukutana navyo, wakihimiza umuhimu wa ujenzi wa vyoo bora katika jamii na matumizi yake.

Hata wale ambao wamebatatika kujenga vyoo, huwa ni vya kienyeji vikiwa si imara, visivyo na paa wala mlango, hali ambayo ni hatari kwa afya au wakati kusababisha ajali kutokana na kutokuwa imara.

Kuna haja ya jamii kuendelea kuelimishwa, ili itambue kuwa vyoo bora vinasaidia kuimarisha afya, hivyo ni vyema kila mtu awe na huduma hiyo nyumbani kwake badala ya kutegemea vichaka au choo kibovu.

Inatajwa kuwa, kaya zenye vyoo bora nchini, zimefikia asilimia 63.7 mwaka 2020, kutoka asilimia 59 ya mwaka 2019, huku lengo likiwa ni kufikia mwaka 2030, hakuna anayejisaidia ovyo katika mazingira yasiyo rasmi.

Mikoa inayotajwa kuongoza kwa kuwa na asilimia kubwa ya kaya zenye vyoo bora ni Dar es Salaam (95.8), Iringa (77.5) na Njombe (74.6), huku mikoa yenye hali duni ikiwa ni Kigoma (49.3), Lindi (49.2) na Dodoma (46.1).

Mkurugenzi wa Huduma za Kinga Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Dk. Leonard Subi, anaweka wazi hayo siku ya Matumizi ya Choo Duniani na Wiki ya Usafi wa Mazingira Tanzania.

Inaaminika kwamba, juhudi zaidi za kuelimisha umma wa Watanzania na hasa wa maeneo ya vijijini kutambua umuhimu wa kujenga vyoo bora zinahitajika.

Yawezekana, sababu kubwa ya maeneo hayo kukosa vyoo imara inatokana na ukosefu wa elimu ya afya au hali duni ya maisha ambayo inawafanya watu wakose fedha za kujenga vyoo vya aina hiyo.

Kama hizo ndizo sababu zinazochangia hali hiyo, itapendeza kama wale ambao hawajui umuhimu wa vyoo wakaelimisha, lakini pia wasio na uwezo wa kifedha, wanaweza kusaidiwa kujengewa vyoo hivyo.

Huduma hiyo ni ya faragha ambayo ni muhimu mtu kuwa na staha, kuliko ambavyo imekuwa ikifanywa na baadhi ya watu kwenda kujidhalilisha vichakani, kwenye maji au katika mabonde.

Inaaminika kwamba, jamii ikiendelea kuelimishwa juu ya huduma hiyo, itatambua kuwa matumizi ya vyoo ni muhimu, kwa kuwa inaimarisha afya na kuiwezesha kutekeleza majukumu yao vizuri.

Elimu ya usafi mazingira ni kinga ya magonjwa ya mlipuko, hivyo jamii ikifahamu hilo na kuchukua hatua, kuna uwezekano wa kila kaya kuwa na choo bora, ambacho itakuwa inakitumia.

Vilevile, elimu inapotolewa kwa wingi, vyoo bora vitaongezeka katika jamii na hatimaye kuachana mila potofu za kuamini kwamba si sahihi kujisaidia chooni au mtindo wa kwenda haja katika mazingira yasiyo rasmi.

Suala la kuhimiza jamii kujenga na kutumia vyoo bora na kunawa mikono kwa maji na sabuni mara baada ya kupata huduma hiyo, vinapusha kupata maambukizo ya magonjwa ya mlipuko.

Wataalamu wa afya wanasema, kuumwa tumbo kunakotokana na ulaji wa chakula, amiba, kama taifodi, homa ya matumbo na magonjwa ya kuhara damu, yanaweza kukoma kwa kuwa yanasababishwa na uchafu wa mazingira.

Msisitizo uliopo ni kuwa na vyoo bora na kuvitumia, vinavyoepusha kuwapo kwa hatari hiyo, kwa kuwa hakutakuwa na mtu anayejisaidia vichakani, majini na mabondeni.


twiga cement
HEIDELBERGCEMENT Group

# AUDITED RESULTS
## FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2020

**CHAIRMAN'S STATEMENT**

Despite many challenges posed in the year 2020, Tanzania Portland Cement Public Limited Company (TPCPLC) delivered a strong operating result when compared to the year 2019. Turnover and sales volume increased by 13% and 6% respectively. The increased revenue combined with disciplined cost management led to the operating profit of 104.9BTZS.

The operating performance of the plant and availability of the machinery was good, ensuring clinker production reached record levels, all within an environment where the Health and Safety of our employees and contractors is paramount. The continued focus on maintaining excellent customer relations and producing high quality products enabled TPCPLC to again demonstrate its strength as the leading player in the industry.

| INCOME STATEMENT | 2020 TZS'000 | 2019 TZS'000 |
|---|---|---|
| Revenue | 393,739,557 | 348,828,076 |
| Cost of sales | (258,416,416) | (229,954,588) |
| **Gross profit** | **135,323,141** | **118,873,488** |
| Other operating income | 2,250,391 | 4,293,998 |
| Selling and administrative expenses | (2,942,285) | (2,746,244) |
| Administrative expenses | (25,976,365) | (26,629,390) |
| Other operating expenses | (3,709,781) | (6,536,148) |
| **Operating profit** | **104,945,101** | **87,255,704** |
| Financial items | 2,484,133 | (1,380,718) |
| **Profit before tax** | **107,429,234** | **85,874,986** |
| Taxes on income | (32,752,864) | (26,171,702) |
| **Profit for the year** | **74,676,370** | **59,703,284** |
| Other comprehensive income , net of tax | 1,028,800 | (988,050) |
| **Total Comprehensive Income** | **75,705,170** | **58,715,234** |
| Number of Shares | 179,923,100 | 179,923,100 |

| BALANCE SHEET | 2020 TZS'000 | 2019 TZS'000 |
|---|---|---|
| **ASSETS** | | |
| Intangible fixed assets | 797,216 | 849,314 |
| Tangible fixed assets | 134,429,769 | 137,094,378 |
| Right of use assets | 4,198,644 | 7,430,771 |
| Non-current financial assets | 1,346,000 | 5,905,187 |
| **Non.current assets** | **140,771,629** | **151,279,650** |
| Inventories | 52,404,781 | 61,598,827 |
| Trade and other receivables | 55,571,973 | 52,006,440 |
| Other current financial assets | 600,000 | 4,721,453 |
| Cash and cash equivalents | 103,855,770 | 72,684,693 |
| **Current assets** | **212,432,524** | **191,011,413** |
| **TOTAL ASSETS** | **353,204,153** | **342,291,063** |
| **EQUITY & LIABILITIES** | | |
| **Equity** | **255,000,767** | **231,473,296** |
| Lease liabilities | 1,,231,231 | 3,097,244 |
| Long term provisions | 6,337,102 | 7,620,008 |
| Provision for deferred taxes | 14,273,690 | 17,573,518 |
| **Non-current liabilities** | **21,842,023** | **28,290,760** |
| Lease liabilities | 3,725,915 | 4,974,507 |
| Current income tax payable | 1,013,768 | 1,027,428 |
| Trade and other payables | 68,765,217 | 73,307,570 |
| Dividend payable | 2,856,463 | 3,217,502 |
| **Current liabilities** | **76,361,363** | **82,527,007** |
| **TOTAL EQUITY & LIABILITIES** | **353,204,153** | **342,291,063** |

**Prospects**

The cement demand in Tanzania and in the East-African region has been growing steadily in recent years. TPCPLC is well placed to meet this growing demand and will continue to work to maintain its market leadership and position.

**Dividend**

The Board proposes a dividend for year 2020 of TZS 390. The Register of Members will close on 10 May 2021, and the last day of trading cum dividend will be 5 May 2021. The dividend will be paid on or about 30 June 2021.

**Appreciation**

The Board would like to thank all its stakeholders for their support during the past year. We have every confidence that TPCPLC will continue to deliver value for the shareholders in the future.

BY ORDER OF THE BOARD

Hakan Gurdal
Chairman of the Board
14.04.2021

**Tanzania Portland Cement Public Limited Company**
**P.O.Box 1950**
**Dar-es-salaam**
**Tanzania**
**www.twigacement.com**
**Email: info@twigacement.com**

# Bank of India (Tanzania) Ltd.

*Relationships beyond banking*

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)**

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA KWA UMMA

"Dortmund hawataki kumuuza Haaland na hakuna vita kati yangu na Dortmund," alisema Raiola akinukuliwa na gazeti la Bild.

Raiola ameelezea kuwa; "Ninaweza kuthibitisha kuwa nilikuwa Dortmund. Mkurugenzi wa Michezo – Michael Zorc, aliweka bayana kuwa hawataki kumuuza Erling. Nina heshimu hilo, lakini haimaanishi ninakubaliana nalo. Hakuna vita kati yangu na Dortmund."

## Real Madrid wamfuatilia Kane




**MADRID,** Hispania

REAL Madrid wanafuatilia kwa ukaribu nyendo za nyota wa Tottenham, Harry Kane na uwezekano wa Spurs kumuuza mshambuliaji huyo kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

Nahodha huyo wa England, Kane anaripotiwa kujiandaa kufanya mazungumzo na Mwenyekiti wa Spurs, Daniel Levy na kocha Jose Mourinho, katika jitihada za kuzungumzia hatma yake klabuni hapo.


Taarifa zinaeleza kuwa Kane hafurahii kuwapo Spurs na anataka kupata mahali pengine ambako kutakuwa na ushindani zaidi, akiamini timu hiyo haijawa na ushindani wa kutosha kwenye Ligi Kuu England.

Hii inatajwa kuwa ndiyo itakuwa sababu ya yeye kuondoka kuelekea msimu ujao wa 2021/22.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa na gazeti la Mundo Deportivo, Levy na Mourinho wote wanajiandaa kumuuza Kane, lakini hawatataka kuboresha moja ya wapizani wao wa Ligi Kuu England na hivyo wanataka kumuuza nje ya Uingereza.

Hii inawafanya Real Madrid kuwa kwenye nafasi nzuri ya kufufua nia yao ya awali ya kumnasa nyota huyo mwenye umri wa miaka 27, wakati Spurs wakimpa thamani ya kati ya pauni milioni 120 hadi 150 ambalo kimsingi linakuwa ni dili la bei nafuu ukifananisha na Erling Haaland kutoka Borussia Dortmund kwa eurao milioni 180.

## Neto nje msimu mzima



**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Wolves, Pedro Neto, anatarajiwa kuwa nje ya uwanja kwa muda wa msimu wote uliobaki kutokana na majeraha ya goti aliyoyapata kwenye mchezo dhidi ya Fulham.

"Neto alipata majeraha ya kifundo cha goti wakati wa mechi na Fulham," ilieleza taarifa ya Wolves.

"Atakuwa nje ya uwanja kwa kipindi chote cha msimu huu kilichobaki," ilisema taarifa ya klabu hiyo baada ya ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Fulham Ijumaa iliyopita

Pedro amecheza mara 35 akiwa na Wolves msimu huu, huku akifunga mabao matano na kutoa pasi za mwisho tano.

Wolves pia wataendelea kukosa huduma ya beki wao Johny na Marcal ambao bado wapo chumba cha majeruhi.

Huku kiungo wao, Reuben Neves akipimwa kukutwa na maambukizi ya virusi vya corona na hivyo atakuwa nje ya kikosi kwa muda wa wiki mbili.

Wolves hawajawa na mwenendo mzuri sana wa uchezaji wao, huku wakiwa na alama 38 katika nafasi ya 12, wakishinda mechi 10 na kupoteza 13.

Wolves watacheza na Sheffield United Jumamosi hii bila ya nyota wao hao wanne.

Letshego

# LETSHEGO BANK (T) LIMITED

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA 31.12. 2020

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2020

(Kiasi kwa millioni shilingi )

| (Kiasi kwa shilingi '000) | | 31-Dec-20 Iliyokaguliwa | 31-Dec-19 Iliyokaguliwa |
|---|---|---|---|
| **A. MALI** | | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 638 | 411 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 6 070 | 3 011 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 342 | 201 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 17 | 13 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa Kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 27 793 | 25 916 |
| 12 | Mali Nyingine | 1 800 | 2 336 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za Udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1 973 | 1 474 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **38 633** | **33 362** |
| **B. DHIMA** | | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 4 224 | 3 175 |
| 18 | Amana za Wateja | 9 753 | 7 057 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa fedha Tslimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana Maalumu | 0 | 0 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 0 | 0 |
| 23 | Limibikizo za Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 0 | 46 |
| 24 | Dhima la Tozo Kwaajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Meneja | 0 | 0 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo | 0 | 0 |
| 27 | Dhima Nyingine | 1 041 | 1 953 |
| 28 | Madeni | 6 811 | 8 253 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **21 828** | **20 484** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 KUTOA 20)** | **16 805** | **12 878** |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 45 007 | 38 457 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | -25 579 | -22 723 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | -2 623 | -2 856 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 0 | 0 |
| 36 | Stahiki ya wenye Hisa Chache | 0 | 0 |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **16 805** | **12 878** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 39 | Mikopo chechefu (Zaidi ya Siku 30) | 4 122 | 5 457 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 4 427 | 5 562 |
| 41 | Mali nyingine chechefu | - | - |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 43% | 39% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 13% | 16% |
| | | 0% | 0% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 231% | 308% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 72% | 77% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 97% | 99% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 37% | 0% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 16% | 0% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.12.2020

(Kiasi kwa shilingi '000)

| *(Kiasi kwa shilingi '000)* | | 31-Dec-20 Iliyokaguliwa | 31-Dec-19 Iliyokaguliwa |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 7 106 | 8 400 |
| 2 | Gharama za Riba | (1 639) | (1 724) |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2) | 5 467 | 6 676 |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | (1 382) | (3 489) |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la Tengo katika Mikopo | 493 | 2 872 |
| **6** | **Mapato yasiyo na Riba** | 545 | 800 |
| | 6.1 Faida/(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 7 | (96) |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 535 | 811 |
| | 6.3 Gawio | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 4 | 85 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba** | (7 708) | (7 956) |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (4 272) | (4 391) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - |
| | 7.3 Gharama nyingine | (3 436) | (3 565) |
| **8** | **Faida / (Hasara) ya Uendeshaji** | (2 585) | (1 097) |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (38) | (1 603) |
| **10** | **Faida / (Hasara) Hasili Baada ya Kodi ya Mapato** | **(2 623)** | **(2 700)** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumulisha (bainisha) | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa** | **(2 623)** | **(2 856)** |
| **13** | **Idadi ya Waajiriwa** | 128 | 145 |
| 12 | Mapato kwa Hisa | N/A | N/A |
| 13 | Mapato ya Hisa zilizochujwa | N/A | N/A |
| **14** | **Idadi ya Matawi** | 5 | 5 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -7% | -8% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa fedha za wanahisa | -9% | -10% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | -121% | -102% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazo Zalisha | 20% | 24% |

Signed by:

**Andrew Tarimo**
(Mkurugenzi Mtendaji)

**Rashid Sendoro**
(Mkaguzi wa ndani)

**Lydia Machangu**
(Meneja wa Fedha na Utawala)

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uendeshaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikuwa na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha mwaka sasa,

**Simon Jengo**
Chairman

**Geofrey Mramba**
Director

Sisi, tuliotajwa hapo juu, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benk na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006, nazinaonesha hali halisi.

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA ULIOISHIA 31.12.2020

(Kiasi kwa millioni shilingi )

| Mwaka wa Sasa 2020 | | Mtaji wa Hisa | Mtaji utokanao na hisa za upendeleo | Tengo la Ziada ya Jumla | Ziada ya Kisheria | Hasara Kusanyiko | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | | **29 937** | **8 520** | **0** | **0** | **-25 579** | **12 878** |
| 1 | Mapatao mengine yaliyojumuishwa | 5 132 | - | - | - | - | 5 132 |
| 2 | Tengo la ziada ya Jumla | 1 418 | - | - | - | - | 1 418 |
| 3 | Ziada Ya Kisheria | - | - | - | - | - | - |
| 4 | Mengineyo - ( IFRS -9) | - | - | - | - | - | - |
| 5 | Faida /(Hasara) baada ya kodi ya mapatao | - | - | - | - | - | - |
| 6 | Mengineyo | - | - | - | - | (2 623) | (2 623) |
| 7 | | | | | | | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | | **36 487** | **8 520** | **-** | **-** | **(28 202)** | **16 805** |
| **Mwaka Uliopita 2018** | | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | | 29 237 | 8 520 | 291 | 0 | -23 014 | 15 034 |
| 1 | Mapatao mengine yaliyojumuishwa | 700 | - | - | - | - | 700 |
| 2 | Transfer to general Provision reserve | - | - | (291) | - | 291 | - |
| 3 | Tengo la ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - |
| 4 | Ziada Ya Kisheria | - | - | - | - | - | - |
| 5 | Faida /(Hasara) baada ya kodi ya mapatao | - | - | - | - | - | - |
| 6 | Mengineyo | - | - | - | - | (2 856) | (2 856) |
| 7 | | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | | **29 937** | **8 520** | **-** | **-** | **(25 579)** | **12 878** |

TANGAZO

# CITIBANK TANZANIA LIMITED

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | 2020 TZS '000 | 2019 TZS '000 |
|---|---|---|
| Mapato ya Riba | 31,302,946 | 34,374,542 |
| Gharama za Riba | (12,191,777) | (10,580,178) |
| **Mapato Halisi ya Riba** | **19,111,169** | **23,794,364** |
| Ada na Kamisheni | 4,645,837 | 6,234,137 |
| Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 8,822,446 | 9,735,059 |
| **Jumla ya Mapato** | **32,579,452** | **39,763,560** |
| Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 149,649 | (188,618) |
| **Jumla ya Mapato baada ya Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo** | **32,729,101** | **39,574,942** |
| Mishahara na Mafao | (7,974,742) | (9,826,203) |
| Uchakavu wa Mali | (1,905,423) | (659,508) |
| Gharama za kiutawala | (15,479,588) | (14,512,927) |
| | **(25,359,753)** | **(24,998,638)** |
| Faida /(Hasara) ya Uendeshaji | 7,369,348 | 14,576,304 |
| Tengo la Kodi ya Mapato | (2,312,847) | (4,406,371) |
| **Faida Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **5,056,501** | **10,169,933** |
| **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa** | | |
| – Mapato ambayo hayajakamilika | 231,840 | 642,133 |
| – Tengo la Kodi ya mapato ambayo hayajakamilika | (69,552) | (192,640) |
| **Mapato mengine baada ya kodi ya mapato** | **162,288** | **449,493** |
| **Jumla ya Faida iliyojumuishwa** | **5,218,789** | **10,619,426** |

### VIASHIRIO VYA UFANISI

| | 2020 | 2019 |
|---|---|---|
| Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Fedha za Wanahisa | 5.11% | 9.80% |
| Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Mali | 0.38% | 1.17% |
| Uwiano wa gharama na mapato | 77.84% | 63.17% |
| Uwiano wa mapato halisi ya riba kwa mali zinazozalisha | 1.67% | 3.11% |
| Uwiano wa Mapato yasiyo ya riba kwa Pato | 41.34% | 40.16% |
| Uwiano wa Mikopo kwa amana za wateja | 27.34% | 44.27% |
| Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 0.00% | 0.00% |
| Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 85.76% | 88.19% |
| Ongezeko la Mali | 53.70% | -5.99% |
| Ongezeko la Mikopo Halisi kwa wateja | 5.63% | 69.95% |
| Ongezeko la Amana za wateja | 71.06% | -11.69% |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2020

| | Mtaji wa Hisa TZS '000 | Akaunti nyingine za mtaji TZS '000 | Mapato Yaliyobakizwa TZS '000 | Tengo la ziada ya kisheria TZS '000 | Tengo la ziada ya jumla TZS '000 | Jumla TZS '000 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa mwaka 1 Januari 2020** | 9,659,900 | 1,597,049 | 92,611,318 | - | - | 103,868,267 |
| Faida Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 5,056,501 | - | - | 5,056,501 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | 162,288 | - | - | - | 162,288 |
| **Jumla ya Faida iliyojumuishwa kwa mwaka** | **-** | **162,288** | **5,056,501** | **-** | **-** | **5,218,789** |
| Gawio litakalolipwa | - | - | (10,169,934) | - | - | (10,169,934) |
| Hamisho la Tengo la Ziada | - | - | (1,582,094) | 1,582,094 | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31 Desemba 2020** | **9,659,900** | **1,759,337** | **85,915,791** | **1,582,094** | **-** | **98,917,122** |

| | Mtaji wa Hisa TZS '000 | Akaunti nyingine za mtaji TZS '000 | Mapato Yaliyobakizwa TZS '000 | Tengo la ziada ya kisheria TZS '000 | Tengo la ziada ya jumla TZS '000 | Jumla TZS '000 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa mwaka 1 Januari 2019** | 9,659,900 | 1,147,556 | 92,054,612 | - | 2,386,773 | 105,248,841 |
| Faida Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 10,169,934 | - | - | 10,169,634 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | 449,493 | - | - | - | 449,493 |
| **Jumla ya Faida iliyojumuishwa kwa mwaka** | **-** | **449,493** | **10,169,934** | **-** | **-** | **10,619,127** |
| Gawio lililolipwa | - | - | (12,000,000) | - | - | (12,000,000) |
| Hamisho la Tengo la Ziada | - | - | 2,386,773 | - | (2,386,773) | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31 Desemba 2019** | **9,659,900** | **1,597,049** | **92,611,318** | **-** | **-** | **103,868,267** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | 2020 TZS '000 | 2019 TZS '000 |
|---|---|---|
| **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| Faida ya Uendeshaji | 7,369,348 | 14,576,304 |
| *Marekebisho kwa Ajili ya:* | | |
| Uchakavu wa Mali | 1,905,423 | 659,508 |
| Uchakavu wa haki ya matumizi ya mali | 640,895 | 1,398,645 |
| Faida/(hasara) ya mapato mengine yaliyojumuishwa -mali | 42,446 | (44,413) |
| Faida/(hasara) ya mapato mengine yaliyojumuishwa -dhima | 25,618 | (38) |
| Gharama za tengo katika mikopo | (23,012) | (230,267) |
| Mapato Halisi ya Riba | (19,111,169) | (23,794,364) |
| Faida juu ya uuzaji wa mali na vifaa | (29,208) | - |
| | **(9,179,659)** | **(7,434,625)** |
| **Mabadiliko katika shughuli za uendeshaji wa mali na madeni** | | |
| Mikopo Halisi kwa wateja | (16,971,700) | (124,153,485) |
| Amana za benki nyingine | (52,634,829) | 51,757,522 |
| Uwekezaji wa Amana za Serikali | 5,514,341 | 863,159 |
| Hifadhi ya chini ya kisheria | (9,333,574) | 9,952,676 |
| Mali Nyingine | (21,973,713) | 18,849,449 |
| Amana za Wateja | 485,095,659 | (90,329,638) |
| Dhima Nyingine | 25,203,007 | (16,641,702) |
| **Fedha iliyozalishwa kutokana na shughuli za uendeshaji** | **405,719,532** | **(157,136,644)** |
| Riba iliyopokelewa | 31,302,946 | 34,374,542 |
| Riba iliyolipwa | (12,191,777) | (10,580,178) |
| Kodi iliyolipwa | (2,703,497) | (4,763,497) |
| **Fedha Halisi zilizotumika kwa shughuli za uendeshaji** | **422,127,204** | **(138,105,777)** |
| **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji** | | |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (1,261,294) | (1,392,957) |
| | 29,208 | - |
| **Fedha Halisi Zilizotumika kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(1,232,086)** | **(1,392,957)** |
| **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha** | | |
| Malipo kwa ajili ya dhima ya kukodisha | (1,181,304) | (1,393,721) |
| Gawio lililolipwa | - | (12,000,000) |
| **Fedha Halisi Zilizotumika kwa Shughuli za Kifedha** | **(1,181,304)** | **(13,393,721)** |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Mwaka** | **329,592,135** | **482,484,590** |
| Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji | 422,127,204 | (138,105,777) |
| Fedha Halisi Zilizotumika kwa Shughuli za Uwekezaji | (1,232,086) | (1,392,957) |
| Fedha Halisi Ziilizotumika kwa Shughuli za Kifedha | (1,181,304) | (13,393,721) |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Mwaka** | **749,305,949** | **329,592,135** |

### WARAKA MIZANIA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | 2020 TZS '000 | 2019 TZS '000 |
|---|---|---|
| **MALI** | | |
| Fedha Taslimu na Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 133,165,746 | 70,972,698 |
| Mikopo Halisi kwa benki | 674,660,811 | 307,636,432 |
| Chombo cha kifedha kinachotokana na Mali | 2,121 | 44,567 |
| Uwekezaji katika Amana za Serikali | 150,449,567 | 155,732,071 |
| Mikopo Halisi kwa wateja | 319,223,382 | 302,210,380 |
| Mali Nyingine | 38,356,233 | 16,400,809 |
| Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 9,210,251 | 9,854,380 |
| Mali ya kodi ya kampuni | 698,929 | 208,172 |
| Haki ya matumizi ya mali | 5,180,568 | 1,398,645 |
| Malipo ya kodi yanayotarajiwa baadae | 3,093,162 | 3,262,819 |
| Hundi na miamala ya Kushughulikiwa | 243,262 | 413,300 |
| **JUMLA YA MALI** | **1,334,284,032** | **868,134,273** |
| **DHIMA** | | |
| Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 904,063 | 53,538,892 |
| Amana za Wateja | 1,167,796,367 | 682,700,708 |
| Chombo cha kifedha kinachotokana na Dhima | 25,618 | - |
| Dhima Nyingine | 61,995,778 | 26,622,836 |
| Dhima ya kukodisha | 4,645,084 | 1,403,570 |
| **JUMLA YA DHIMA** | **1,235,366,910** | **764,266,006** |
| **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 9,659,900 | 9,659,900 |
| Akaunti Nyingine za Mtaji | 1,759,337 | 1,597,049 |
| Tengo la ziada ya jumla | 1,582,094 | - |
| Mapato Yaliyobakizwa | 85,915,791 | 92,611,318 |
| **Jumla ya fedha za wanahisa** | **98,917,122** | **103,868,267** |
| **Jumla ya fedha za wanahisa na dhima** | **1,334,284,032** | **868,134,273** |

Taarifa hizi zilipitishwa na Bodi ya Wakarugenzi tarehe 31 Machi 2021 na kutiwa saini kwa niaba yake na::

Geofrey Mchangila
**Ofisa Mtendaji Mkuu**

Andulile Mwakalyelye
**Mjumbe wa Bodi**

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2014, na zinaonesha hali halisi.

Godwin Rutashobya
**Mkaguzi Mkuu wa Ndani**

Yande Panya
**Mjumbe wa Bodi**

Andulile Mwakalyelye
**Mjumbe wa Bodi**

# Michezo

Alhamisi Aprili 15, 2021

Nipashe




RAIOLA: DORTMUND HAWAMUUZI HAALAND HABARI UK 21

UTAKUBALI TU...



Winga wa Simba, Luis Miquissone, akipiga hesabu za kumtoka Kiungo wa Mtibwa Sugar, Abubakar Ame, katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jana na Simba kushinda mabao 5-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## MWAMBUSI AWABADILISHIA DOZI MASTRAIKA YANGA SC

**Na Saada Akida**

IMEKWISHA! Hayo ni maneno ya Kaimu Kocha Mkuu wa Yanga, Juma Mwambusi, ambaye amesema amewapa 'programu' maalumu washambuliaji wake ili watumie vema nafasi za kufunga zitakazopatikana katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo imezidi kuwa ngumu.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mwambusi alisema kila idara katika timu hiyo haikosi upungufu, lakini kwa sasa ameimarisha nguvu na mipango kwa washambuliaji wake ambao anahitaji pia waongeze umakini wanapokaribia lango la wapinzani.

Mwambusi amesema wanafanya kazi kubwa ya kutengeneza nafasi, lakini umaliziaji umekuwa ni tatizo linalowatafuna mastraika wake na kikosi hicho.

"Hizi nafasi ni muhimu sana kuhakikisha zinatumika vizuri, kwa sababu ligi imeshakuwa ngumu, mechi iliyopita dhidi ya KMC, tulishindwa kupata ushindi kwa sababu hatukuzitumia vema nafasi tulizozitengeneza na kulazimisha sare.

"Lazima tupambane kupata ushindi katika michezo iliyokuwa mbele yetu, hakuna kingine ambacho tunakitafuta kwa sasa ni kupigania pointi tatu kila mechi iliyopo mbele yetu," alisema kocha huyo.

Alisema malengo waliyokuwa nayo kwa sasa ni kupambana kutafuta pointi muhimu katika michezo iliyobakia ikiwamo dhidi ya Biashara United ambao watacheza Jumamosi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

# Simba yabisha hodi kileleni

### Yazamisha mkono mzima kwenye mfuko wa sukari ya Mtibwa, Kagere naye amshusha Dube mbio za Kiatu Ligi Kuu Bara huku...

**Na Adam Fungamwango**

MABAO mawili yaliyofungwa na Mnyarwanda Meddie Kagere, Wazambia Clatous Chama na Rally Bwalya na lingine la Luis Miquissone raia wa Msumbiji, yalitosha kuilaza na 'viatu' Mtibwa Sugar kwa kichapo cha 5-0 katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana.

Kwa ushindi huo mnono iliyoupata Simba katika mechi yake hiyo ya 21 msimu huu, inaifanya kupanda nafasi ya pili ikifikisha pointi 49, pointi mbili tu nyuma ya kinara wa Ligi Kuu, Yanga yenye alama 51, lakini yenyewe ikiwa mbele kwa mechi tatu huku Azam iliyoshuka dimbani mara 25, ikishuka hadi nafasi ya tatu na pointi zake 47.

**Lakini mabao hayo mawili ya Kagere yamemfanya kukwea kileleni na katika orodha ya wafungaji, akifikisha mabao 11, akimpita Mzimbabwe Prince Dube wa Azam FC aliyecheka na nyavu mara 10.**

Simba ilianza biashara mapema tu dakika ya nane ilipoandika bao lake la kwanza kupitia kwa kiungo wake Chama, ambaye alipiga mkwaju wa faulo uliokwenda moja kwa moja wavuni.

Faulo hiyo ilitokana na Miquissone kuchezewa vibaya nje kidogo ya eneo la hatari, mfungaji akiupeleka mpira kulia kwa golikipa Aboutwalib Mshery.

Dakika 10 baadaye Bwalya alipeleka mpira upande ule ule wa kulia aliopeleka Mzambia mwenzake kwa kipa na kuipatia Simba bao la pili, baada ya krosi safi iliyochongwa na Shomari Kapombe.

Mtibwa walifanya mashambulizi mawili ya hatari dakika ya 30 na 31 wakati George Makang'a alipowatoka mabeki wa Simba na kubaki na kipa Aishi Manula, lakini akapiga shuti kubwa juu huku mwenzake Ally Makarani akiwa anaomba apasiwe afunge, lakini pia Jaffar Kibaya aliikosesha timu yake bao alipopiga mpira nje baada ya pasi safi kutoka kwa Haruna Chanongo.Alikuwa ni Kagere alipoandika bao la tatu dakika ya 42, baada ya kuwahadaa mabeki wa Mtibwa, akageuka na kupiga shuti hafifu la chini, lakini la ufundi lililokwamia wavuni na kuandika bao la tatu.

Kagere tena, dakika tano baada ya mapumziko, aliwainua vitini mashabiki wa Simba kwa kupachika bao la nne alipopata pasi safi kutoka kwa Bwalya ambaye naye alipokea pasi kutoka kwa Miquissone.

Miquissone, alipigilia msumari wa mwisho kwenye 'jeneza' la Mtibwa kwa kupachika bao la tano, alipopokea pasi safi ya kisigino kutoka kwa Chama, akapiga mpira kwa ufundi, uliokatika na kujaa wavuni.

Baada ya mabao hayo, wachezaji wa Simba walionekana

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002